Nipashe
Jumanne Aprili 16, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581648
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Masauni** aonya wanaotumia mitandao kijamii vibaya UK.3



**TBS** yahadharisha unywaji pombe bila kipimo UKURASA 4

**ACT**- Wazalendo yalia na serikali 3 UK. 19



**ARTETA: VIJANA SIMAMENI NAFASI ARSENAL BADO IPO** UKURASA 21

## RIPOTI YA CAG

# Ulaji bado upo

UKURASA 2, 3 & 19




Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake jijini Dodoma jana, kuhusu taarifa yake ya ukaguzi wa fedha za serikali kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30 2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Nchimbi kukipeleka kikokotoo kwa Rais

- **Kinana:** Uchaguzi hautakuwa rahisi... *Ukurasa 5*



**MICHEZO** **MO AFANYA KIKAO KIZITO MECHI YANGA** UK.24 **MAONI,** UK.6



Naibu Waziri wa Fedha, Hamadi Hassan Chande akiweka mezani ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu ukaguzi wa taarifa za fedha za serikali kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2023, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

RIPOTI YA CAG

# Ulaji bado upo

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, imeonesha kuwa ununuzi na usimamizi wa mikataba katika mamlaka 35 za serikali za mitaa wa jumla ya Sh. bilioni 4.22 ulifanyika bila kuitisha nukuu za ushindanishi wa bei.

Aidha, mamlaka 16 za serikali za mitaa, zenye ununuzi wa jumla ya Sh. bilioni 4.87 ziliamua kutumia njia ya mzabuni mmoja au wachache badala ya njia ya ushindanishi bila sababu za kuridhisha.

Hayo yamo kwenye ripoti kuu ya mwaka wa ukaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/23, ambayo pia ilibaini mamlaka 13 za serikali za mitaa zilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 1.45 ambazo hazikupokewa licha ya malipo kufanyika.

**HASARA KITUO CHA MABASI**

"Kuhusu usimamizi wa mikataba, ilibainika kuwa mkandarasi na mkandarasi mshauri waliohusika na usimamizi wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi cha Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam kilichopo Mbezi Luis, walikuwa hawajalipwa ankara zao za jumla ya Sh. bilioni 8.92, hivyo kusababisha madai ya riba ya Sh. bilioni 2.23," alisema.

**MFUMO WA TAUSI**

CAG alibaini pamoja na kuanzishwa kwa Mfumo wa Ukusanyaji Mapato Serikalini (TAUSI) na maelekezo mahususi kwa mamlaka za serikali za mitaa kusajili mashine za kukusanyia mapato (POS), kufanya usuluhishi wa wadaiwa kwenye mfumo wa awali wa LGRCIS, na kutumia moduli zote ndani ya TAUSI kwa ukamilifu, bado kuna Sh. bilioni 45 ambazo ni madai ya mapato yasiyokusanywa kwenye mfumo.

**UKUSANYAJI MAPATO**

Aidha, alibaini jumla ya Sh. bilioni 61 hazikukusanywa na mamlaka 130 za serikali za mitaa, kutoka vyanzo mbalimbali kama vile kodi ya maduka, vibanda vya soko, kodi ya nyumba, mauzo ya viwanja, ukusanyaji wa taka, leseni za biashara, leseni za vileo, maeneo ya wazi yaliyokodishwa, ada za maegesho, na vyanzo vingine vya mapato, ikiashiria kukosa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

"Katika kupitia taarifa za mifumo ya LGRCIS na TAUSI, nilibaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 6.2 ambazo ni mapato yaliyokusanywa kupitia mashine za POS katika mamlaka za serikali za mitaa 96, hazikuwa zimewasilishwa benki za mamlaka za serikali za mitaa husika."

"Usimamizi wa matumizi tathmini yangu ya usimamizi wa akaunti ya amana unaofanywa na mamlaka za serikali za mitaa ulibua kasoro kadhaa zenye jumla ya Sh. bilioni 10.71 katika akaunti za amana zinazomilikiwa na mamlaka za serikali za mitaa," ilibainisha ripoti hiyo.

**MADAI WAZABUNI**

Ripoti hiyo ilibainisha kuwa katika mamlaka za serikali za mitaa 37 kuongezeka kwa madai ya wazabuni na wafanyakazi kutoka Sh. bilioni 64.87 kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi Sh. bilioni 87.32 kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikiashiria ongezeko kubwa la Sh. bilioni 22.45, sawa na asilimia 35.

Kuhusu usimamizi wa rasilimali watu katika mamlaka 54 za serikali za mitaa, alibaini madai ya watumishi yenye jumla ya Sh. bilioni 36.47 ambayo hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12.

Madai hayo yanajumuisha malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi, stahiki za wastaafu, na stahiki zingine kama vile posho za kisheria kwa wakuu wa idara na vitengo.

Ulinganifu wa taarifa za mishahara kutoka kwenye Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu (HCMIS) na kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ulibaini utofauti mkubwa.

"Mathalani, utofauti wa tarehe za kuzaliwa ulibainika kwa watumishi 77,286 katika takwimu za kanzidata zote mbili, na kusababisha mkanganyiko kuhusiana na tarehe sahihi za kuzaliwa kwa watumishi wa umma. Nilibaini kuwa hapakuwa na takwimu zozote za watumishi 86 katika kanzidata ya NIDA," alisema.

Aidha, alisema tathmini yake ya mifumo ya uhasibu wa Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) ambao umechangia katika dosari zilizobainika wakati wa ukaguzi wa miamala iliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe na kubaini malipo ya jumla ya Sh. bilioni 1.23, yalifanywa kupitia akaunti ya mishahara kwa shughuli ambazo hazikufanyika.

**MIRADI YA MAENDELEO**

Mamlaka za serikali za mitaa 20 zenye miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 8.04 ambayo imekamilika, lakini haitumiki, na kutofikiwa malengo yaliyokusudiwa.

Vilevile, CAG alibaini dosari mbalimbali katika miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 13.81 iliyotekelezwa na mamlaka 14 za serikali za mitaa.

**ELIMU BILA MALIPO**

Ufanisi wa uendeshaji sekta ya elimu katika mwaka wa fedha 2022/23, ulikuwa na upungufu wa ruzuku ya elimu bila malipo iliyotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa 15 kwa ajili ya shule za msingi na sekondari, ikiwa jumla ya Sh. bilioni 1.25 kati ya Sh. bilioni 11.83 zilizokuwa zimepangwa katika bajeti ya kipindi hicho.

CAG alisema TAMISEMI ilitoa jumla ya Sh. bilioni 10.6 kwa Taasisi ya Elimu Tanzania kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya shule za msingi, ambayo iliingia mkataba na kampuni nne za uchapaji na usambazaji wa vitabu milioni 2.51, lakini hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha usambazaji wa vitabu hivyo.

**MIRADI BILA EIA**

Mbali na hayo, CAG amebaini miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 635.12 ilianza bila kuwa na cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira (EIA) na kijamii, wakati ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 7.12 kwa taasisi 15 ulifanyika bila kuidhinishwa na bodi za zabuni.

Pia amebaini upungufu kwenye michakato ya utoaji zabuni, ambapo taasisi 16 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 149.56 bila kutumia mfumo wa kielektroniki.

Kadhalika, taasisi sita zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 77.67 bila kutumia njia za ushindani wa bei. Ununuzi wa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 2.16 ulifanyika bila kutumia mikataba na mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.78 haikupekuliwa na wanasheria.

Amebaini upungufu katika kutimiza majukumu ya kimkataba ambapo taasisi 11 zilichelewa kulipa madai ya Sh. bilioni 38.73 na kutolipa madai ya Sh. bilioni 19.37 ndani ya muda uliokubaliwa.

Wizara ya Ujenzi haijalipa riba ya Sh. bilioni 17.48 iliyotokana na uamuzi wa usuluhishi uliofikiwa tangu mwaka 2014 pamoja na riba ya Sh. bilioni 34.82 iliyotozwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kuchelewa kulipa makandarasi.

Pia mikataba 46 ya ujenzi ilikosa dhamana za utendaji kazi zenye thamani ya Sh. bilioni 383.76.

CAG pia amebaini Tume ya Madini na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) hazikudai dhamana ya utendaji kazi na malipo ya awali yenye thamani ya jumla Sh. milioni 675.90 kwenye mikataba iliyositishwa.

HABARI KITAIFA

## Masauni aonya wanaotumia vibaya mitandao kijamii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, ameonya watu wanaotumia vibaya mitandao ya kijamii kutukana viongozi wakuu wa serikali na kwamba hakuna mtu atakayefanya uhalifu asichukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya miaka 60 ya Muungano, Masauni alisema serikali haitamfumbia macho mtu yeyote atakayebainika kuvunja sheria za nchi bila kujali cheo chake.

"Hakuna mtu yeyote ambaye atavunja sheria halafu serikali imuache tu bila kumchukulia sheria kwani hakuna aliye juu ya sheria bila kujali nafasi yake," alisema.

Aliwataka Watanzania kuendelea kutii sheria na kuacha kujihusisha na mambo yanayovunja sheria za nchi kwenye mitandao ya kijamii.

Masauni alisema serikali imeridhia kuanzishwa kwa kibali cha hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania na kwa sasa Idara ya Uhamiaji inakamilisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji sura ya 54 ili kuwezesha hadhi hiyo kisheria.

Alisema kutolewa kwa hadhi hiyo kutasaidia kuimarisha mahusiano baina ya serikali na kundi hilo kwa kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba fursa hiyo tofauti na wageni wengine ambao hawana nasaba au mafungamano na nchi.

Pia, alisema katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji haramu wa binadamu, imesadia waathirika 1,338 waliokuwa wakitumikishwa ndani na nje ya nchi na kati yao 1211 waliokolewa hapa nchini na waathirika 127 waliokolewa kutoka nchi za nje.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

## Mpango aagiza Wizara Ardhi kulinda bustani za kijani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, ameiagiza Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchukua hatua za kulinda maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya bustani za kijani ili yasiharibiwe au kubadilishwa matumizi.

Dk. Mpango alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akifungua Kongamano la Jukwaa la Maendeleo Endelevu, kuhamasisha uwekezaji katika bustani za kijani kwa maendeleo endelevu.

Alisema, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinapaswa kuchukua hatua za kulinda maeneo yote yaliyotengwa nchini kwa ajili ya bustani za kijani.

Alisema, kutokana na changamoto zilizopo maeneo mengi yaliyotengwa kwa ajili ya bustani za kijani katika miji na majiji nchini yameharibiwa na mengine kubadilishwa matumizi kinyume na mipango miji.

"Pia mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe kuwa zinatunga sheria ndogondogo ambazo zitatumika kulinda maeneo haya ili yasiharibiwe wala kubadilishwa matumizi yake," alisema.

Aliitaka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kuanzisha tuzo maalum ya kushindanisha bustani bora za miji na majiji.

Kadhalika, aliuagiza mkoa wa Dodoma kabla ya mwisho wa mwaka huu kuwa na bustani tatu za kijani.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 56 ya Watanzania wanaishi mjini na kama hatua hazitachukuliwa hali itazidi kuwa ngumu.

# Mamilioni Mfuko wa Wanawake hayajarejeshwa kwa miaka 20

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini Sh. milioni 664.50 hazijarejeshwa kwa muda wa miaka saba hadi 20 kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Pia amebaini kampuni ya ulinzi ya Suma JKT na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji hawajakusanya jumla ya Sh. bilioni 1.86 walizopaswa kukusanya.

Vilevile, vituo vinne vya ukaguzi wa afya katika mipaka, bandari na viwanja vya ndege vilishindwa kukusanya tozo za ukaguzi Sh. milioni 879.11 baada ya ukaguzi huku Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi (PHAB) ikishindwa kukusanya Sh. milioni 768 kutoka kwenye vituo vya afya 2,640 vilivyosajiliwa upya.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka 2022/23 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa jana, CAG Charles Kichere anabainisha kuwa Mfuko wa Wanawake ulitoa mikopo ya Sh. bilioni 1.13 kwa vikundi vya wanawake na watu binafsi bila kuikatia bima na kati yake, mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 664.5 haijarejeshwa.

### BIL 32/- ARDHI

CAG anasema Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pia imeshindwa kukusanya Sh. bilioni 32.43 zilizotolewa kwa halmashauri ili kutekeleza mipango ya upimaji na umilikishwaji hati miliki za ardhi baada ya kumalizika kwa muda wa urejeshwaji fedha hizo Juni 30, 2022.

Katika hospitali za rufani, CAG amebaini kuwa hospitali nne zilishindwa kukusanya Sh. milioni 452 kwa kushindwa kufuatilia fedha za matibabu ya wagonjwa wanaotumia bima za mifuko mingine, wakati Sh. milioni 111.76 hazikukusanywa baada ya hospitali tatu za rufani kutoa misamaha ya gharama za matibabu kwa wagonjwa wasio na sifa za kupata misamaha ya matibabu.

Pia amebaini Sh. bilioni 61.09 hazikukusanywa na taasisi 29 licha ya kutoa huduma. Fedha hizo zimeripotiwa kama madai huku Sh. bilioni 4.058 katika akaunti za taasisi tano za serikali zikikaa muda mrefu bila kutumiwa na Sh. bilioni 7.73 zilikusanywa na taasisi tatu nje ya mifumo ya ukusanyaji.

### MKATABA TATA

Vilevile, CAG amebaini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) iliingia makubaliano ya upangishaji eneo la ardhi lenye mita za mraba 11,000 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), jijini Dar es Salaam kwa shughuli za kibiashara kwa masharti nafuu yanayopelekea ukusanywaji mdogo wa mapato ya serikali, malipo ya pango kwa mita mraba yalikuwa Dola za Marekani 4.36 tangu mwaka 1995 hadi mwaka 2018, ambayo yalipunguzwa hadi dola za Marekani 4.09 kwa mita mraba.

### UKIUKWAJI KANUNI

CAG pia amebaini taasisi saba zimekiuka kanuni za fedha kwa kuwa na bakaa ya Sh. bilioni 2.45 katika akaunti zao za matumizi za masurufu huku 13 zikifanya malipo ya Sh. bilioni 2.87 bila kudai stakabadhi za kielekitroniki kutoka kwa wauzaji bidhaa na watoa huduma.

Pia ukarabati wa jengo la ofisi ya Balozi Kampala, Uganda haujaanza licha ya kuwa na bakaa ya Sh. bilioni 1.78 tangu mwaka 2018 na kumekuwa na gharama kubwa za kodi ya pango ya Sh. bilioni 18.46 kwa majengo ya ofisi na makazi katika balozi 39 za Tanzania nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

### DOSARI MSD

CAG pia amebaini Bohari ya Dawa (MSD) ilinunua mashine 10 za kuondoa maumivu, ukakamavu na mkazo wa misuli kwa bei ya Sh. milioni 136.7 na kuacha kununua vifaa hivyo kwa mzabuni aliyebainika kuwa na bei ndogo wakati wa ushindani ya Sh. milioni 103.2, hivyo kusababisha gharama za ziada ambazo zingeepukika za Sh. milioni 33.5.

Mdhibiti amebaini ununuzi wa vifaatiba kwa wazabuni 32 waliopewa zabuni zenye thamani ya Sh. bilioni 4.14 bila kufanyiwa uchambuzi wa awali na kuidhinishwa na bodi ya zabuni.

Pia amebaini vifaatiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 13.37 ambavyo ununuzi wake haukuwa umeanza. Amebaini uchelewaji ununuzi na usambazaji vifaatiba katika vituo vya afya kwa siku zinazoanzia 23 hadi 1,458 tangu fedha zilipopokewa na bohari hadi vifaatiba vilipofika kwenye vituo vya afya, vituo 21 vya afya vilipokea vifaa vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.68 ambavyo vilikuwa havijaanza kutumika.

# TBS yatoa angalizo wanywaji pombe kuzingatia vipimo

**Restusta James na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetoa angalizo kwa wanywaji pombe nchini kuzingatia vipimo vinavyotakiwa, ili kuepuka madhara ikiwamo magonjwa ya figo.

Limesema limekuwa likifanya udhibiti wa vilevi visivyo na ubora vinavyotoka nje ya nchi na zinazotengenezwa nchini, lakini tatizo ni wanywaji kutofuata maelekezo ya matumizi ya vinywaji hivyo.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Ubora wa TBS, Lazaro Msasalaga, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano na waandishi wa habari kuhusu utendaji wa taasisi hiyo.

Kwa mujibu wa Shirika la Health Direct, kinywaji aina ya wine chenye kilevi cha asilimia 13 mtu anapaswa kunywa mililita 100 (sawa glasi moja), bia yenye kilevi cha asilimia 4.9 (mililita 285, sawa na chupa tatu), pombe kali yenye kilevi cha asilimia 40 (mililita 30, glasi toti moja), pombe zitokanazo na matunda zenye kilevi cha asilimia 4.9 (mililita 285).

Msasalaga alisema kwa sasa kuna matumizi mabaya ya kinywaji cha 'enegy drink' na pombe kali, watumiaji wengi wanatumia bila kufuata maelekezo.

"Utakuta mtu anakunywa wakati hajala, mwingine anakunywa kuzidi kiwango kinachotakiwa, mwisho wa siku anaumwa figo halafu anasema ni pombe feki," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema TBS katika utekelezaji wa majukumu, imepata mafaniko mbalimbali ikiwamo kujenga maabara katika mikoa ya kimkakati ambayo ni Dodoma inahudumia mikoa ya Tabora na Singida.

"Shirika linatarajia kuanza ujenzi wa maabara ya kisasa katika Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Kanda ya Kaskazini (Arusha). Maabara ya Kanda ya Ziwa inatarajiwa kuhudumia mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Geita, Shinyanga na Simiyu. Maabara ya Kanda ya Kaskazini inatarajiwa kuhudumia mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara," alisema Dk. Ngenya.

Alitaja mafanikio mengine ni ununuzi wa mashine za kisasa za maabara kwa kutumia fedha za ndani pamoja na misaada kutoka kwa wadau wa maendeleo.

Kuhusu mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara, Dk. Ngenya alisema katika kipindi cha miaka mitatu, viwango 1,721 vya kitaifa viliandaliwa Pamoja na kushiriki katika uandaaji wa viwango vya kibiashara Afrika Mashariki na Afrika.

Alisema serikali kwa kupitia TBS imekuwa ikitenga zaidi ya Sh. milioni 250 kwa ajili ya kuwahudumia wajasiriamali wadogo bila malipo.

"Kwa kipindi cha miaka mitatu, leseni za ubora wa bidhaa 2,106 zilitolewa kwa wazalishaji mbalimbali wa bidhaa hapa nchini. Kati ya leseni hizo, 1,051 zilitolewa bure na kwa wajasiriamali wadogo.

Dk. Ngenya alisema kwa kipindi cha miaka mitatu, wadau 5,789 kutoka mikoani walipewa mafunzo ya ujasiriamali.

Alisema TBS imeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo na wazalishaji ili kuwawezesha kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama na hatimaye kukidhi ushindani wa masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

Vilevile, alisema kwa kipindi cha miaka mitatu, leseni za ubora wa bidhaa 2,106 zilitolewa kwa wazalishaji mbalimbali wa bidhaa.

Kuhusu ukaguzi wa bidhaa kutoka nje, Dk. Ngenya alisema kwa kipindi cha miaka mitatu shehena 100,851 zilikaguliwa kabla hazijaingizwa nchini, bidhaa 151,570 kutoka nje ya nchi zilikaguliwa baada ya kufika nchini.

Kuhusu usajili wa bidhaa za vyakula na vipodozi, Dk. Ngenya alisema kwa kipindi cha miaka mitatu shehena 100,851 zilikaguliwa kabla hazijaingizwa nchini.

Pia, alisema bidhaa 151,570 kutoka nje ya nchi zilikaguliwa baada ya kufika nchini.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Athumani Ngenya (kulia), akizungumza na waandishi wa habari wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya shirika hilo katika kipindi cha miaka mitatu ya serikali ya awamu ya sita, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: CARLOS BANDA**

# Mbunge ataka Tume Huru Uchaguzi Zanzibar

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Konde (ACT-Wazalendo), Mohammed Said Issa, ameitaka serikali kuifanyia mabadiliko Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kama ilivyofanyika kwa Tume ya Uchaguzi Tanzania ili kuondoa udanganyifu unaofanyika visiwani humo wakati wa uchaguzi.

Mbunge huyo alisema licha ya serikali kufanyia marekebisho Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kuibadili kuwa Tume Huru ya Uchaguzi bado kwa upande wa Zanzibar inatambulika kama Tume ya Uchaguzi Zanzibar na kudai kuwa hakuna kilichobadilika kwa upande huo.

Alisema ili uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na uchaguzi mkuu ufanyike kwa uhuru na haki, ipo haja ya serikali kubadili Tume hiyo ili nayo iwe huru na kufanya kazi chini ya sheria mpya iliyopitishwa na Bunge na kusainiwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Bunge hili limepitisha na Rais tayari ametia saini na ni sheria tayari licha ya kuwa sheria hii inatumika kama ya Tanzania ila huku Zanzibar bado wakala anayetumika ni yuleyule inatakiwa naye afanyiwe marekebisho ili yasijitokeze tena yale ya uchaguzi uliopita," alisisitiza.

Kuhusu uwajibikaji wa Tume hiyo, aliitaka kuwajibika ipasavyo ili kuondoa udanganyifu alioutaja kutokea katika uchaguzi wa marudio wa madiwani katika maeneo mbalimbali nchini akiutaja kutokuwa huru.

**SERIKALI KUNUNUA MAHINDI**

Wakati huo huo, serikali imewataka wakulima wote nchini pamoja na wafanyabiashara kuacha kuuza mazao kwa bei ya hasara ndani na nje ya nchi na kuwa ipo tayari kununua mazao hayo kwa bei elekezi ili kuacha kuwaumiza wakulima.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati akichangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2024/25 na kueleza kuwa kwa sasa serikali imeruhusu kuuza mazao kwa nchi jirani, lakini sio kwa bei inayomuumiza mkulima,

Aidha, aliwataka wakulima wa mahindi ambao tayari wameanza kuvuna kutokukimbilia kuuza mahindi yao kwa bei rahisi kwa kuwa serikali inakaribia kuanza kununua na wafanyabiashara wote wana maelekezo namna ya kuuza mahindi katika nchi zenye uhitaji mkubwa.

"Tunawaruhusu wauze kwa nchi jirani zenye matatizo ya chakula,lakini hatutawaruhusu kuuza mahindi kwa bei ya kutupwa kwani atakayepata hasara ni mkulima kwahiyo tumewaelekeza haya na tayari tumeanza kuwapa vibali vya usafirishaji nje. Tumekubaliana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na tuwauzia unga badala ya mahindi na tumeanza kusaga jumla ya tani 30,000 hivyo tuwaondoe hofu juu ya mavuno makubwa mtakayokuwa nayo," alisema.

MAPOROMOKO MLIMA

# RC apiga marufuku ugawaji viwanja bila idhini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU moja baada ya kutokea maporomoko ya tope lililofunika nyumba 20 na shule moja katika Kata ya Itezi jijini Mbeya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amepiga marufuku maofisa ardhi kupima viwanja katika eneo lolote kabla Kamati ya Mipango Miji haijaidhinisha.

Aidha, amepiga marufuku upimaji wa viwanja kwenye maeneo yote hatarishi yakiwamo ya pembezoni mwa mito ambayo inaweza kufurika na kusababisha madhara kwa binadamu.

Homera alitangaza marufuku hiyo alipotembelea eneo lililoathirika na maporomoko hayo ambayo yalisababishwa na kumeguka kwa Mlima Kawetere kutokana na mvua ya masika inayoendelea kunyesha jijini humo.

Alisema nyumba zilizoathiriwa na tope hilo zina hatimiliki zilitolewa na jiji hilo na kwamba endapo kamati ya mipangomiji ingekagua eneo hilo kabla ya kuanza kumilikisha watu kuna uwezekano ingezuia madhara hayo.

"Maeneo yote hatarishi ni marufuku kupima viwanja kuanzia sasa, ni lazima kamati ya mipango miji ijiridhishe kwanza kuhusu usalama wa eneo husika ndipo upimaji uendelee," alisema Homera.

Hata hivyo, viongozi wa mila wameiomba serikali kuwasikiliza wanapotoa maoni yao kuhusu maeneo yanayopimwa kwa ajili ya makazi wakidai kuwa baadhi ya maeneo yana historia ambazo sio za kawaida.

Katibu wa machifu wa Jiji la Mbeya, Michael Ilanga, alisema eneo hilo maporomoko yalianzia miaka ya nyuma paliwahi kuwapo ziwa dogo ambalo baadaye lilipotea na miaka ya karibuni limerejea tena likiwa na umbo dogo.

Alisema pia kuna mambo ya kimila yalikuwa yanafanywa na moja ya familia kutokana na ndugu yao kupotelea kwenye ziwa hilo miaka ya nyuma kwa kuzama.

Hata hivyo, alisema chanzo cha mlima huo kumeguka ni kukatwa kwa miti iliyokuwa imepandwa na kuruhusu shughuli mbalimbali za kibinadamu, ikiwamo kilimo na ujenzi wa makazi kwenye maeneo hayo ya miinuko.

"Hapa zamani palikuwa na miti ambayo ilipandwa na jiji, lakini walikata miti hiyo na wakapima viwanja, sasa tumekuwa tukitoa maoni yetu, lakini yanapuuzwa, hata pale Mwansekwa viwanja vimepimwa milimani," alisema Chifu Ilanga na kuongeza.

"Hili eneo pia kuna nyoka na wanyama wengine wadogo, nawaomba wananchi mkimuona huyo nyoka wala kinyonga msiwapige acheni wataondoka wenyewe, tunajua sisi namna tutakavyowaondoa," aliongeza chifu.

Baadhi ya viongozi wa dini walishauri kwenye maeneo ya miinuko kusifanyike shughuli zozote za kibinadamu, ikiwamo kilimo na ujenzi wa makazi ili kuepuka majanga.

Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya Mkoa wa Mbeya, Sheikh Ayas Njalabaha, alisema kwenye vitabu vitakatifu milima imetajwa kuwa nguzo ya kuzuia udongo kuporomoka na hivyo kitendo cha wananchi kuharibu mazingira kwenye maeneo hayo ndiyo chanzo cha mapotomoko.

HABARI KITAIFA

# Nchimbi kukipeleka kikokotoo kwa Rais

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Emmanuel Nchimbi, ameahidi kufikisha kilio cha kikokotoo kwa Rais Samia Suluhu Hassan, huku Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara, Abdulrahman Kinana akiwatahadharisha wananchama wa chama hicho kuwa, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani utakuwa wa ushindani na kuwataka wasibweteke.

Viongozi hao walitoa kauli hizo jana kwa nyakati tofauti wakiwa katika mwendelezo wa ziara zao mkoani Rukwa na Mara.

Akiwa mkoani Rukwa, Dk. Nchimbi aliwaahidi wastaafu na watumishi waliopo kazini kwamba atawasilisha kero ya kikokotoo kwa Rais Samia kwa ajili ya utatuzi, akisisitiza imekuwa kero kubwa kwa wastaafu.

Dk. Nchimbi alisema: “Tatizo la kikokotoo linalalamikiwa sana na watumishi, imekuwa kero kubwa, kuna muda lazima tuangalie wananchi wetu, wanachama wetu, tuangalie tutafika wapi, lakini kwa kadri inavyowezekana tunapaswa kutatua kero za wananchi.”

Aliongeza: “Nitalifikisha suala hilo katika uongozi wa juu kuona namna ya kulitafutia ufumbuzi kwakuwa lengo la CCM ni kutatua kero za wananchi.”

Pamoja na mambo mengine, Dk. Nchimbi aliwataka waliopewa zabuni ya kujenga Uwanja wa Ndege wa Rukwa kuongeza kasi ili kuendana na matakwa ya mkataba.

Aliwataka viongozi wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), mradi huo unajengwa kwa ubora, akiwahimiza kutanguliza uzalendo kwa maslahi ya taifa.

Alisema kwa mujibu wa mkataba uwanja huo unapaswa kukamilika ndani ya miezi 18, lakini mpaka sasa ni asilimia nane pekee zimekamilika.

Pia, aliahidi kuwasiliana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kutatua tatizo la uhaba wa madaktari bingwa mkoani Rukwa.

Kadhalika, aliwataka wanachama wa CCM kuchagua viongozi wenye sifa, huku akisistiza katika uchaguzi kuna kushinda na kushindwa.

Akijibu hoja ya mmoja wa wanachama wa CCM aliyetaka mabalozi wa shina wa chama hicho walipwe mshahara, Dk. Nchimbi alisema suala hilo haliwezekani kwa sababu wao ndiyo wenye chama.

Hata hivyo, alisema mazingira yatakaporuhusu watapewa kifuta jasho na wasipopata wajue hali ya chama sio nzuri.

Naye Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM, Amos Makalla, alipokea kero 57 na kuagiza uongozi wa mkoa kuzipitia na kumrejeshea majibu.

Katibu wa NEC Oganaizesheni CCM, Issa Gavu, aliwataka viongozi walioko ndani ya chama kujituma kwa kuwatumikia wananchi sambamba na kujenga utamaduni wa kusikiliza kero zao.

Pia, aliwataka wajumbe wa mashina ya CCM kujenga utamaduni wa kukaa vikao vya kila mwisho wa mwezi na kwamba hilo litaleta chachu ngazi ya tawi kutimiza majukumu yao.

UCHAGUZI

Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana akiwa mkoani Mara aliwaonya wanachama wa chama hicho kutobweteka, kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa mwakani utakuwa mgumu.

Akizungumza jana katika kikao cha wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Rorya, mkoani Mara, alilisisitiza kufuatwa kwa maadili ya uchaguzi.

“Zile sheria za uchaguzi zilizotungwa bungeni zinatoa nafasi ya ushindani, kwa hiyo msibweteke, badala yake tujipange vizuri. Tunatakiwa tujipange wanachama ili tupate ushindi wa kishindo mwaka huu pamoja na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025,” alisema Kinana.

Alisema kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni vema wana CCM wakashikamana na endapo kuna mtu mchana yuko upande wa CCM na usiku upinzani anapaswa kuwekwa kando haraka.

Kuhusu viongozi walioko madarakani wakiwamo madiwani na wabunge, Kinana alisema waachwe wafanye kazi akieleza kuwa hakuna sababu ya kuwavuruga kwa sababu kipindi cha uchaguzi bado hakijafika.

Pia, alikemea tabia ya ukabila akisema ni mambo ya kizamani na yanawagawa.

Kinana alisema nchi kuwa na makabila ni jambo la kawaida ila ukabila ni jambo baya.

Alisema Baba wa Taifa Hayati Julius Nyerere alitoka Mkoa wa Mara moja ya kabila dogo na ameongoza nchi kwa miaka 24, alipendwa, aliheshimiwa, alithaminiwa na alitukuzwa sio kwa sababu ya ukabila bali ni kazi aliyokuwa anafanya, utendaji na uadilifu wake uliomfanya aheshimike Tanzania, Afrika na duniani.

***Imeandaliwa na Halfani Chusi (Rukwa) na Maulid Mmbaga (Rorya)**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
16.04.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya Jumatano tarehe **17-04-2024 hadi tarehe 20-04-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero kupitia Mikumi,** gari hizo zina namba za usajili:
   **T 204 DYJ /T 877 EAU**
   **T 478 ECF /T 568 EAZ**

   Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

   | | | |
   |---|---|---|
   | **Urefu** | - | **mita 24.00** |
   | **Upana** | - | **mita 5.10** |
   | **Kimo** | - | **mita 5.60** |

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero** kupitia **Mikumi,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
*Facilitating Partnerships for Development*

**JOB VACANCY**

## GRADUATE RECRUITMENT ANNOUNCEMENT

**About FCS**

Foundation for Civil Society (FCS) is a leading Tanzanian not-for-profit development organization that provides grants and capacity building support to local civil society organizations (CSOs). Established in September 2002, FCS has become one of the largest sources of funding for small and medium-sized Tanzanian CSOs and one of the most prominent and credible civil society institutions in Africa. Our mission is to contribute to sustainable and inclusive development in Tanzania through strengthening capabilities and sharing resources. We achieve this through strategic partnerships with CSOs, community groups, and other development actors. Over the years, FCS has supported more than 5,500 CSOs in all 31 regions of Tanzania, both in Mainland and Zanzibar. Through these efforts, we have reached millions of people and significantly contributed to good governance processes.

The FCS Graduate Interns Program is a unique opportunity for recent graduates to gain valuable work experience, make a tangible impact in the development sector, and kick-start their careers with a respected organization. This program is designed to attract talented individuals who possess the skills and the passion to contribute meaningfully to FCS' mission. We are looking for graduates (graduated in 2022 or later) with diverse skills ready to immerse themselves in the work of a thriving non-profit.

*Individuals can apply in the following Internship Areas*

**Creative Production**

Skilled in video production, photography, graphic design, etc. Ability to translate concepts into compelling visual content.

**General Communications**

Strong writing skills, social media savvy, ability to plan and execute events, passion for engaging with diverse audiences.

**Data and Research**

Proficient in data analysis tools, statistical packages, and research methods, ability to gather and interpret data to inform strategic decisions.

**Programs**

Passion for development issues, ability to write activity concepts and reports, strong organizational skills, excellent cross-functional communication. Knowledge and interest in climate change and gender issues will be an added advantage.

**Finance and Admin**

Interest in financial management, administrative support, and logistics. Attention to detail, problem-solving attitude, and desire to support organizational efficiency.

*Qualifications:*

- Bachelor's degree in a relevant field, aligned with the desired traineeship area, completed in 2022 or later. Applicants with demonstrated academic excellence (such as high GPA scores and/or academic awards) are encouraged to apply.
- Demonstrable skills and experience through coursework, projects, internships, or volunteer work.
- Strong interest in civil society development, social impact, and contributing to positive change in Tanzania.
- Exceptional written and verbal communication skills in both English and Swahili.
- Ability to work both independently and collaboratively in a dynamic team environment.

*We Value:*

- Enthusiasm and a proactive approach to learning on the job.
- Creativity, innovation, and a willingness to explore new ideas.
- Potential for growth and a desire to make a lasting contribution to FCS.

*What we offer:*

- 12-month internship with the potential for conversion to a permanent or consulting position based on performance.
- On-the-job training and mentorship from experienced FCS staff.
- Opportunities to work on real-world projects and contribute to FCS deliverables.
- A monthly stipend to facilitate transport and meals.

**Mode of Application**

- Apply via Foundation for Civil Society (FCS) Linkedin page through the link https://www.linkedin.com/jobs/view/3895068601/?refId=TJV3JAzZ31lfxZErFF%2FkFw%3D%3D
- The deadline for submission is **26 April 2024** at **16.00hrs**.

**Apply now**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wananchi hatari hii mnayoikimbilia mpaka lini?

**KUMEKUWA** na kawaida kila inapotokea jambo la hatari wananchi kuwa na kawaida kulimbilia badala ya kujiepusha nalo.

Hili limetokea mara kadhaa, licha ya elimu kutolewa mara kwa mara, lakini bado wananchi wanaonekana kuziba masiko au kujifanya hawaoni.

Askari wa Usalama Barabarani kila mara wanatoa elimu watu kuacha kukimbilia ajali ili kuepusha majanga zaidi yasitokee, lakini wananchi wanaamua kujitoa mhanga.

Miaka kadhaa iliyopita kulitokea ajali ya lori la mafuta na wananchi walikimbilia kuchota mafuta bila kujali hatari inayoweza kuwapata na ajali hiyo ilishuhudiwa watu wengi wakipoteza maisha. Haikupita miaka mingi, ajali nyingine ya lori la mafuta ikatokea mkoani Morogoro na kwa staili ile ile, wananchi wakaikimbilia ili kwenda kuchota mafuta.

Kilichotokea kwenye ajali hiyo kila mtu atakuwa anakumbuka. Watu wengi walipoteza maisha na wengi wakabaki na ulemavu wa maisha.

Serikali imejitahidi kutoa elimu mara kwa mara kuwaonya watu kuacha kukimbilia ajali zinazotokana na malori ya mafuta kwa sababu hatari yake ni kubwa wakati wowote yanaweza kulipuka.

Wakati machungu ya kumbukumbu ya ajali hizo hayajapotea, juzi eneo la Miyomboni, Kata ya Misugusugu, wilayani Kibaha, mkoani Pwani, ilitokea ajali ya lori la mafuta kuacha njia na kupinduka.

Kitendo cha lori hilo kupinduka, kiliwaamsha baadhi ya wananchi wanaoishi eneo hilo na wale wa karibu kwenda kuchota mafuta na kuondoka nayo bila kujali kuwa kuna binadamu wenzao waliokuwa ndani ya lori hilo ambao walikuwa wakihitaji msaada wa kuokolewa.

Kila mmoja alikuwa anakimbilia achote mafuta ili aende kuyauza, hakufikiria kuwa kitendo hicho ni hatari kingeweza kuhatarisha maisha yao.

Cha kumshukuru Mungu ni kwamba ajali hiyo haikuleta madhara kama zilivyotokea ajali nyingine zilizohusisha malori ya mafuta.

Wananchi bado wanahitaji elimu na kukumbushwa kila wakati athari ya kukimbilia ajali kwa sababu wanachoangalia ni namna watakavyopata pesa kutokana na kile wanachokwenda kukichukua.

Gharama inayotokana na ajali kama hizo ni kubwa kuliko hata hiyo pesa wanayokwenda kupata baada ya kuuza mafuta hayo.

Ugumu wa maisha upo, lakini kutoa rehani maisha yako kwa sababu ya shibe ya siku moja ni jambo linalosikitisha.

Ubinadamu umepotea kabisa, inapotokea ajali wananchi wanachojali ni kukimbilia kuiba mali zilizomo ndani ya magari, hata wanapoona binadamu mwenzao akiomba msaada wa kuokolewa wanamuacha apoteze maisha, wanachothamini ni kile watakachokipata kwenye magari hayo.

Kwa ajali iliyotokea juzi huko Pwani, wananchi walionekana kukimbilia kuchota mafuta wakiwa wamerundikana kila mmoja akiwa amebeba dumu analoona linafaa kubeba mafuta hayo bila kujihurumia.

Kinachosikitisha zaidi inapotokea ajali kama hizo watoto nao hukimbilia na wengine wazazi wao kuwahamasisha kwenda nao ili waweze kupata mafuta mengi zaidi.

Kwa ajali hiyo ya Mkoa wa Pwani, imeelezwa kuwa watu sita wameshakamatwa kwa kuhusika kuchota mafuta na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, amethibitisha kuwa hakuna madhara ya kibinadamu yaliyotokea.

Kwa hilo la kutotokea madhara kwa binadamu ni la kumshukuru Mungu, vinginevyo tungekuwa kwenye msiba mwingine wa kupoteza watu kwa kuungua na mafuta.

Wananchi jiepusheni na kukimbilia majanga, nguvu kazi kubwa inapotea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

## Wanafunzi wasiozingatia kuvaa sare sahihi, lazima sheria ichukue nafasi

**HIVI** karibuni nilifika katika shule moja ya sekondari ya serikali ndani ya Dar es Salaam, kuonana na mkuu wa shule hiyo kwa masuala binafsi.

Nikiwa ofisini mwake, nikaona 'vipande' vingi vya suruali. 'Vipande' hivyo vilikuwa chini kwenye kona ndani ya ofisi hiyo. Baada ya kumaliza kuelezea kile kilichonipeleka shuleni hapo, nilijaribu kumuuliza kuhusu vipande hivyo ni vya nini.

Mkuu huyo wa shule akasema, vimekatwa kutoka kwenye suruali za baadhi ya wanafunzi, ambao wanashona sare kwa kukiuka maelekezo ya shule kwa kuzibana chini kama 'vimodo'.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa shule, kila mwanafunzi anayevaa sare hasa suruali ambayo imepunguzwa vipimo kwa chini na kuwa 'modo', inakatwa kuanzia magotini na kipande kubaki ofisini.

Inapokatwa, upande mmoja wa suruali unaishia magotini na mwingine hadi chini, hivyo inakuwa si rahisi mwanafunzi kwenda nayo shule, analazimika ashone nyingine upya kwa kuzingatia maelekezo ya shule.

Nikirejea kwenye hoja yangu ni kwamba, suala la kuzingatia na kuheshimu utaratibu wa shule ni muhimu, badala ya kila mwanafunzi kujifanyia anavyotaka kwa kushona sare kinyume.

Suala la sare linasisitizwa shuleni na linafuatiliwa kwa makini kuanzia mwonekano wa mwili hadi tabia, kwa sababu ni yote hayo ni ya muhimu kwa maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma.

Wanafunzi wa kike wanatakiwa kusuka nywele mistari sita na siyo zaidi ya hiyo na ikiwa hawezi kusuka mistari hiyo, anatakiwa kunyoa nywele ziwe ndogo za kufaa kuchana kwa kitana kidogo.

Kwa wanafunzi wa kiume, wanatakiwa kunyoa nywele kwa mfumo unaofanana kwa maana ya unyoaji wa nywele zinazofaa kuchana kwa kitana kidogo na si vinginevyo.

Lakini cha kushangaza, baadhi ya wanafunzi wamekuwa wanaenda kinyume na utaratibu huo, ingawa wanajua wazi kuwa ni makosa kutofuata maelekezo ya shule.

Nitoe mfano tu, ni ngumu hata kukuta hasa katika shule za serikali, wanafunzi wamechomekea mashati yao, na baadhi wamezikata inakuwa vigumu kuchomeka.

Nadhani kuna haja ya kuwapo kwa uhusiano mzuri kati ya wazazi na walimu kwenye suala la malezi, ili kudhibiti vitendo ambavyo vinafanywa na wanafunzi wachache wasiojali umuhimu wa elimu

Wazazi wafuatilie watoto wao kwa karibu, kwani inashangaza kama wamewashonea sare, halafu watoto wanakwenda kwa mafundi kupunguza upana ili ziendane na wanavyotaka wao na si matakwa ya shule.

Katika kufanikisha hilo, wazazi, waache mtindo wa kuwafuata walimu na kuwafokea pale watoto wao wanapofanya makosa na kuadhibiwa, kwani mtindo huo unavuruga uhusiano kati ya makundi hayo mawili.

Ikumbukwe kuwa, wanavyovaa kinyume na utaratibu wa shule, ndivyo wanavyoonyesha walivyo kwamba wao ni wa aina gani, hivyo ushirikiano ungesaidia kuwanusuru kutoka katika mazingira hayo.

Imekuwa kawaida kukuta baadhi ya wanafunzi wakiwa vijiweni katika vituo vya daladala wamevaa sare hasa suruali 'mlegezo' na tena zimebana kwa chini, huku wamening'niza vitamba kwenye mifuko ya nyuma. Wengine huenda mbali. Viatu vyao ni jamii ya kandambili, jambo ambalo ni kosa kubwa.

Nadhani si sahihi mwanafunzi ambaye anatarajia kuwa mtaalam, kiongozi na msomi wa baadaye kuwa wa aina hiyo. Ni vyema wakasaidiwa wajitambue na kufuata kile kilichowapeleka shule na wanapokuwa wagumu, lazima utaratibu kama wa yule mkuu wa shule uchukue nafasi.

Inaelezwa na baadhi ya wanafunzi kuwa, wapo wengine katika shule hiyo niliotembelea, ambao katika suruali zao chini wameweka zipu, ili wawapo shule ziwe zinaonekana jinsi taratibu zilivyo.

Lakini, wakishatoka shule tu kila mmoja anavuta zipu, suruali inabana tena chini kama kawaida. Hivyo ingekuwa ni vyema kama hao nao watafuatiliwa ili kuwabaini na kuwachukulia hatua.

Ninajua kuna suala la utandawazi na ugumu wa maisha ambao unafanya wazazi wawe na muda mdogo kufuatilia tabia za watoto wao, lakini kwa hali ya sasa, ipo haja ya kuwafuatilia kwa karibu.

Vilevile, jamii nzima isisahau mila, utamaduni na maadili ili kunusuru kizazi hiki ambacho sasa kila mmoja anaonekana ana maamuzi yake bila kujali kwamba ni kinyume.

# Wakurugenzi wa halmashauri kusimamia taulo za kike shuleni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewaagiza Wakurugenzi wa halmashauri kusimamia fedha zinazotengwa kwa upatikanaji wa taulo za kike shuleni kuwafikia walengwa.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Zainab Katimba, alitoa agizo hilo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Ritta Kabati.

Kabati katika swali la nyongeza aliuliza pamoja na serikali kutenga fedha, kuna malalamiko kwenye shule na kuhoji utaratibu unaotumika fedha zinazotengwa kununulia taulo za kike zinawafikia wahusika.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Katimba alisema fedha hizo zinasimamiwa na Wakurugenzi a m b a o wanapaswa kutekeleza agizo hilo.

Awali, katika swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Nora Mzeru, alihoji nini mpango wa serikali kutenga bajeti kwa ajili ya taulo za kike shuleni.

Naibu Waziri Katimba alijibu kuwa serikali imeendelea kuratibu upatikanaji wa taulo za kike kupitia fedha zinazotokana na ruzuku ya uendeshaji, wadau pamoja na mapato ya ndani ya halmashauri na katika mwaka wa fedha 2022/23, Sh. bilioni 3.16 zilitumika kugharamia taulo hizo.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. bilioni 1.97 zilitoka katika ruzuku ya uendeshaji, Sh. milioni 539 zilitoka katika mapato ya ndani ya halmashauri na Sh. milioni 655 zilitoka kwa wadau mbalimbali.

Mwaka 2023/24, serikali ilitenga Sh. bilioni 2.64 kwa ajili ya kugharamia taulo za kike, kati ya fedha hizo Sh. bilioni 1.06 ni za ruzuku ya uendeshaji na Sh. bilioni 1.58 ni kutoka mapato ya ndani ya halmashauri.

"Hadi Machi, 2024 Sh. bilioni 2.2 zimetumika. Pia, wadau mbalimbali walichangia Sh. bilioni 1.5 na miradi ya shule ya elimu ya kujitegemea ilichangia Sh. milioni 119.5.

"Serikali inaendelea kuzisisitiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatenga bajeti kwa ajili ya upatikanaji wa taulo za kike shuleni," alisema.

# Ufanisi TPA wawezesha kupata hati safi miaka 2

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imesema imeongeza ufanisi katika uandaaji na utoaji wa taarifa za hesabu za Mamlaka na kufanikiwa kupata hati safi kwa miaka miwili mfululizo.

Mafanikio hayo yamekuja baada ya Mamlaka hiyo kukamilisha mradi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ambao hutumika katika kuandaa na kuhifadhi taarifa za kifedha.

Katika taarifa yake jana, Mamlaka hiyo ilisema kaguzi zilizofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kwa miaka mfululizo miwili iliyopita, kumeipa mamlaka hiyo hati safi.

Ilisema TPA chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mkuu wake, Plasduce Mbossa, imefanikiwa kutekeleza kwa mafanikio makubwa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kuwa na mifumo Madhubuti ya TEHAMA inatumika.

Ilisema katika mwaka wa fedha 2022/2023 miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na utekelezaji wa maagizo ya Rais ya kukamilisha mradi wa TEHAMA ambao hutumika katika kuandaa na kuhifadhi taarifa za kifedha.

Ilisema mfumo huo pia huunganisha shughuli za Idara mbalimbali katika kutekeleza majukumu ya kila siku na kwamba unaunganisha idara zote muhimu ikiwamo ya Fedha, Rasilimali Watu, Ununuzi na nyingine.

"Matokeo ya kukamilika kwa mfumo huu, ni sanjari na ufanisi katika uandaaji na utoaji wa taarifa za hesabu za TPA, ambapo mfumo huo umeiwezesha TPA kupata hati safi kwa miaka miwili mfululizo kwa kaguzi zinazofanywa na (CAG)," ilisema.

Aidha, taarifa hiyo ilisema kutokana na matumizi ya mfumo huo, TPA imepata tuzo ya uandaaji bora wa taarifa za hesabu kutoka kwa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Vile vile, mfumo huo umeongeza tija katika udhibiti wa mianya ya upotevu wa fedha, uandaaji wa taarifa mbalimbali kwa wakati, utunzaji wa nyaraka na taarifa za kifedha na rasilimali za taasisi.

Kutokana na kuimarika mifumo ya ukusanyaji imesababisha mapato ya TPA kuongezeka kwa asilimia 27 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/2022.

Ilisema kwa upande wa kuhudumia shehena kumekuwa na ongezeko kubwa kwa upande wa meli na shehena, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 idadi ya meli zilizohudumiwa na Bandari za TPA ziliongezeka na kufikia 4,762 kutoka 4,160 ambazo ni wastani wa ongezeko la asilimia 13.9 kwa mwaka.

Ilisema kiwango cha shehena kilichohudumiwa ni tani milioni 27.8 sawa na wastani wa ongezeko la asilimia 21.7 ya shehena iliyohudumiwa katika mwaka husika ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Aidha, Mamlaka imefanya uboreshaji mkubwa wa miundombinu ikiwamo uundwaji wa mifumo ya TEHAMA, Utekelezaji wa Mradi wa Kimkakati wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP), Uboreshaji wa Bandari Tanga, Upanuzi wa Bandari ya Mtwara, Uboreshaji wa Bandari za Maziwa Makuu.

Ilisema uwekezaji huo mkubwa na ununuzi wa mitambo pamoja na ujuzi kwa wafanyakazi umeongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa Mamlaka ya Bandari kwenye bandari zake zote nchini.


FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
Facilitating Partnerships for Development

## JOB VACANCY

**JOB DESCRIPTION**

**POSITION:** Livelihoods Program Lead
**REPORTS TO:** Head of Programs
**SUPERVISION:** None
**WORKING RELATIONSHIPS:** Receives support from Programs Support Officer (shared resource)

**BROAD FUNCTION**

The Livelihoods Program Lead is a visionary strategist, championing civil society engagement in consumer protection, inclusive and sustainable trade practices, and integrating gender expertise into FCS' programming. This role combines expertise in trade systems with a deep commitment to social equity, leading specific project outputs while also guiding FCS' overall climate change and gender approach.

The job holder is expected to manage the inclusive trade and climate action projects, demonstrating strong leadership and comprehensive project management skills, including conceptualization of initiatives, budgeting, implementation, monitoring, learning, adaptation and reporting. The role requires a proactive approach, exceptional problem-solving skills, and the ability to adapt to changing circumstances, ensuring projects are delivered successfully and contribute to the organization's objectives.

**DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

*Inclusive Trade*

- Conduct research and mapping exercises to identify opportunities and challenges for inclusive trade practices, focusing on women, youth, and PWDs.
- Develop and deliver targeted training programs on sustainable trading, cross-border trade, and business literacy, tailored to the specific needs of marginalized groups, especially women, youth and people with disabilities.
- Design and implement grant programs to support high-potential inclusive trade ventures, emphasizing climate-smart approaches.
- Promote the adoption of tools and technologies, including digital platforms, to enhance access to markets for women, youth, and PWDs.

*Consumer Protection*

- Lead advocacy initiatives to strengthen regulatory frameworks for consumer protection, engaging with policymakers and key stakeholders.
- Design and implement capacity-building programs for National Consumer Advocacy Council (NCAC), Consumer Consultative Councils (CCCs), and other relevant committees
- Collaborate with regional organizations to promote harmonized consumer protection measures across East Africa.

*Additional Responsibilities*

- Serve as the in-house gender expert enabling the organization's staff and partners to carry out gender-inclusive project design, implementation, and evaluation.
- Serve as the in-house climate change expert, guiding FCS' strategic engagement in climate-related initiatives.
- Provide training and capacity-building programs for FCS staff and CSO partners on climate-smart practices and advocacy.
- Forge strategic partnerships with key stakeholders in the climate action space, including government agencies, research institutions, and environmental NGOs.
- Collaborate with the monitoring, learning, and communication unit to document lessons learned and articulate the relevance of FCS' programming to its overall inclusive trade and climate action agenda.
- Support the development of compelling proposals and concept notes addressing the intersection of climate change, and social inclusion, with an emphasis on gender-responsive approaches.
- Perform other duties assigned by the Head of Programs, in consultation and with approval from the Executive Director, contributing to the strategic development of FCS' programming.

**PERSON SPECIFICATIONS**

**Qualifications & Experience**

- Master's degree in international trade, climate change, economics, development studies, or a related field.
- At least 7 years of experience in project management, with a proven track record in trade-related programs or climate action initiatives.
- Experience in conducting research, policy analysis, and advocacy campaigns pertaining to trade and climate change.
- Demonstrated focus on inclusive development strategies and empowerment of women, youth, and PWDs.
- Successful track record in proposal writing and donor engagement.

**Skills & Values**

- Strong analytical skills, with the ability to interpret complex trade and climate related information.
- Exceptional project management skills, ensuring accountability and efficient execution of project plans.
- Adept at navigating complex governmental systems and procedures.
- Excellent written and verbal communication skills, particularly communicating technical information effectively to various audiences.
- Passionate about environmental sustainability and social justice.
- Adaptable and resilient, thriving in a dynamic and evolving programmatic landscape.
- Ability to use contemporary tools and techniques to enhance efficiency and effectiveness in managing programs and relationships.

**Mode of Application**

- If you meet the criteria above, apply via Foundation for Civil Society (FCS) Linkedin page through the link **https://www.linkedin.com/jobs/view/3888474556/?alternateChannel=search&refId=3a182d4f-766e-452d-8a8e-a92c9cae4348&trackingId=AEUgX3IMRl6DoQ6ZIKbrjw%3D%3D**
- The deadline for submission is **26 April 2024** at **16.00hrs**.

**Foundation for Civil Society**
7 Madai Crescent, Ada Estate, Plot No.152
P.O.Box 7192
Dar es Salaam.

*The Foundation has zero tolerance for bribery and corruption. We are committed to Gender Equality and Diversity.*

*The Foundation is also an equal opportunity employer, and therefore, all applicants will receive consideration for employment without regard to race, colour, religion, gender, gender identity or expression, sexual orientation, genetics, disability and age.*

# Bashungwa aiagiza TANROAD kurudisha mawasiliano barabara zilizoharibiwa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amemwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Dar es Salaam, John Mkumbo kufanya tathmini ya maeneo yote yaliyoharibiwa na mvua ya El-Nino, kuhakikisha mawasiliano ya barabara yanakuwapo wakati wote.

Alitoa agizo hilo jana bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Kigamboni, Faustine Ndugulile aliyehoji kuhusu mkakati wa muda mfupi wa serikali katika kukarabati Barabara ya Gomvu- Kimbiji - Pembamnazi.

Akijibu swali hilo, Bashungwa alimwagiza meneja huyo wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam kufika katika barabara hiyo na kufanya tathmini ya maeneo yote yaliyoribika, ili mawasiliano ya barabara yaendelee kuwapo wakati wote.



Bashungwa alisema Barabara ya Gomvu - Kimbiji - Pembamnazi ni sehemu ya Barabara ya Mjimwema - Kimbiji - Pembamnazi (km 49) ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha.

"Kwa sehemu ya Cheka - Avic (km 2) tayari ujenzi umekamilika, kwa sehemu ya Avic - Kimbiji (km 10) taratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi zinaendelea," alisema Bashungwa.

Aidha, alisema ujenzi kwa sehemu iliyobaki ya Kimbiji hadi Pembamnazi itajengwa kulinganana upatikanaji wa fedha.

Kuhusu utekelezaji wa Barabara ya Kibada - Mwasonga (km 41), Waziri Bashungwa alimwagiza mkandarasi kuanza kufanya maandalizi ya ujenzi katika eneo la mradi wakati akiandaliwa taratibu za malipo ya awali.

Kadhalika, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuipatia Wizara ya Ujenzi fedha za dharura, ili kusaidia kufanyika ukarabati katika maeneo ambayo mawasiliano ya barabara yamekatika kutokana na mvua inayoendelea kunyesha nchini.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu, Rais Samia ameipa kipaumbele Wizara ya Ujenzi kwa kutoa fedha nyingi zilizoelekezwa katika ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami pamoja na ukarabati



Mkurugenzi wa Uratibu na Uendeshaji Utafiti wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Bugwesa Katale (kushoto), akizungumza wakati wa mkutano wa kamati ya pamoja ya Ushauri wa Kitaalamu wa Utafiti wa Maendeleo ya tume hiyo, Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkurugenzi wa Hospitali Maalumu ya Taifa ya Magonjwa ambukizi Kibong'oto, Dk. Leonard Subi na Mkurugenzi wa Tehama na Uhaulishaji wa Teknolojia, Dk. Masoud Masoud. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# DC Ngara ataka makandarasi kukamilisha miradi

**Na Judith Julius,** NGARA

MKUU wa Wilaya ya Ngara, Mathias Julius, amewataka makandarasi na wasimamizi wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa kwa ufadhili wa NELSAP kuikamilisha na kukabidhiwa kwa wakati ili iwanufaishe wananchi.

Alitoa maagizo hayo wakati akifanya ziara ya kukagua miradi hiyo pamoja na ujenzi wa soko la Kahaza litakalotumiwa na wananchi wa Wilaya ya Ngara na nchi za jirani za Burundi na Rwanda.

Miradi mingine ni ujenzi wa bweni, bwalo la chakula, na jengo la utawala katika Shule ya Sekondari ya Ngara, na jengo la utawala wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Julius, vilevile, alisikiliza kero za wananchi wanaoishi mji wa Rusumo, walioathiriwa na milipuko iliyotokea wakati wa utekelezaji wa mradi wa umeme unaotengenezwa kwa maji katika mji huo.

Mmoja wa waathiriwa wa milipuko, Christina Gilbert, alisema alipewa fedha za kwenda kupanga ili kupisha ujenzi wa nyumba yake, lakini anadai muda aliolipiwa katika nyumba ya kupanga umeisha na sasa hana pesa nyingine ya kuendelea kumlipa mwenye nyumba. Aliongeza kuwa hadi sasa hajui nini cha kufanya.

Elisha Mtagwa, ambaye pia ni miongoni mwa waathiriwa, alisema alitaarifiwa kuwa ujenzi wa nyumba atakayoishi utakamilika baada ya miezi sita, lakini cha kushangaza haoni dalili yoyote ya kumalizika kwa ujenzi huo na kodi aliyopewa kumlipa anayemiliki nyumba aliyopanga imeisha.

Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo, Kaimu Mratibu wa mradi ya LADP, Mhandisi Antony Lameck, alisema gharama zilizotumika ni Sh. bilioni 7.4.

Mhandisi Leonidas Ntibitanga, alisema atawasilisha taarifa za wananchi hao kwenye menejimenti ya shirika ili kuona namna ambayo wananchi watapatiwa fedha za kuendelea kulipa kodi za nyumba walizopanga wakati wa ujenzi na ukarabati ukiendelea.

Julius aliwataka wakandarasi na wasimamizi wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa kwa ufadhili wa NELSAP kuhakikisha inakamilika na kukabidhiwa kwa wakati ili iwanufaishe wananchi.

## Wabunge wataka dharura kurejesha miundombinu

**Na Vitus Audax,** DODOMA

KUTOKANA na maafa yanayoendelea kusababishwa na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini, Wabunge wameiomba serikali kuweka mpango wa dharura kurejesha miundombinu iliyoharibiwa ambayo kwa sasa imekwamisha shughuli mbalimbali za kiuchumi katika maeneo husika.

Mbunge wa Mlimba, Godwin Kunambi akichangia jana bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2024/25 alisema ni zaidi ya mwezi mmoja tangu miundombinu ya barabara na reli ya Mbinga-Mbeya ikatike hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kurejesha usafiri huo.

Alisema hali hiyo inakwamisha shughuli za kiuchumi za wananchi na wakati mwingine kuwalazimu kutumia gharama kubwa kusafirisha bidhaa zao.

Aliishauri serikali kuongeza nguvu kurejesha miundombinu hiyo kupitia Mfuko wa Dharura ikiwa ni pamoja na kulitumia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kufanyia kazi kwa haraka suala hilo.

Mbunge wa Mafinga Mjini, Cosato Chumi, alisema asilimia kubwa ya wananchi ni wakulima na wanatumia sehemu hiyo kama kujiajiri, lakini katika eneo lake makaravati yameharibiwa hali inayowalazimu wananchi wanaosafirisha mazao kuzunguka na kutumia gharama kubwa kuyasafirisha.

"Mfano pale Mafinga barabara ndogo ya kutoka Uguta kwenda Kikombo karavati limechukuliwa na mvua hizi zinazoendelea kunyesha hivyo wananchi wanaharibikiwa na mali zao huku wanaolazimika kuchukua bidhaa hizo wanatumia gharama kubwa na kupata hasara," alisema Chumi.

Aidha, aliishauri serikali kutumia sheria ya Uwekezaji wa Umma (Public Private Partnerships Act), kuzishirikisha sekta binafsi zisaidie kwenye urejeshaji wa miundombinu ili kuipunguzia mzigo srikali.

Mbunge wa Igalula, Venant Protas, alisema kutokana na madhara yaliyosababishwa na mvua katika jimbo lake umetokea uharibifu mkubwa wa barabara hususani Goweko-Igalula na hali ya usafiri na usafirishaji imekuwa ngumu zaidi.

"Katika barabara hii mwananchi alikuwa akisafiri kwa Sh. 3,500 hadi 4,000 na kusafiri kwa muda wa saa mbili, lakini kwa sasa wanatumia zaidi ya Sh. 20,000 na muda wa zaidi ya saa kumi hali inayosababisha upotevu wa muda pamoja na fedha kwa wananchi na wafanyabiashara," alisema.

Aliishauri serikali kuzitazama barabara zote zinazounganisha uchumi ambazo zimeharibiwa na mvua zifanyiwe kazi mapema ili kurahisisha shughuli za kiuchumi.





## Wafanyabiashara watakiwa kuwalinda walaji

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BARAZA la Ushindani (FCT) limewataka wafanyabiashara kuzingatia misingi halali na kumlinda mnunuzi wa mwisho ili kupunguza malalamiko na migogoro baina yao.

FCT mwishoni mwa wiki iliyopita iliendesha mafunzo kwa wadau wake, wakiwemo wafanyabishara ili kupata uelewa utakaowasaidia kujua haki na wajibu wao ikiwemo kumlinda mlaji katika soko.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Frank Mmbando, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuongeza ufanisi kwenye uzalishaji ikiwa ni pamoja na usambazaji na utoaji wa huduma kwa jamii.

"Baraza limefanya jambo la muhimu sana elimu watakayoipata ni muhimu sana kwani itasaidia kutambua haki na wajibu, kustawisha ushindani, na kuongeza kasi ya uwajibikaji katika soko na kusaidia kutatua migogoro ya kiushindani baina ya wadau," alisema Mmbando

Aliwataka washiriki hao kutumia vizuri baraza hilo kutatua changamoto za biashara zinazoweza kujitokeza kwani ni chombo kinachosimamia haki kwa watu wote.

Ofisa Sheria Mkuu wa FCT, Hasfa Said, alisema kati ya kazi zinazofanywa na baraza hilo ni kupokea, kusikiliza na kuamua rufaa zinazotokana na maamuzi ya mamlaka za usimamizi na udhibiti pamoja na tume hiyo ya ushindani.

Alisema baraza hilo linatekeleza sheria ya ushindani ya Bunge na kanuni zake za mwaka 2012.

Aliwataka wafanyabiashara kutumia baraza hilo kwa ajili ya kuwalinda walaji na kuhakikisha wanapata ufanisi katika soko na kukuza uchumi wa nchi.

Mkuu wa Idara ya Uchumi wa FCT, Kulwa Msogoti, alisema baraza hilo linahamasisha wafanyabiashara, wawekezaji, watoa huduma na walaji kupeleka malalamikom kama hawajaridhika na maamuzi yanayotolewa na Tume ya Ushindani na vyombo vya udhibiti.

Alisema baraza hilo linawahamasisha wadau wote wanapodai haki wanatakiwa kutumiza wajibu wao na kufuata sheria za nchi hususani katika biashara na udhibiti wa soko.

Mwenyekiti wa Daladala wa Jiji la Arusha, Maulid Abdallah, alisema kuna mambo mazuri yameelezwa na baraza hilo ikiwemo haki kumlinda mlaji utaratibu wa kuendesha uchumi wa nchi kwa sekta mbalimbali.

Ofisa Mdhibiti Ubora wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Dismoso Chimbunde, alisema lengo la kuhudhuria mafunzo hayo ni kufahamu namna gani ya kukuza na kuwaendeleza wafanyabiashara nchini.

Kaimu Ofisa Huduma kwa Wateja na Utawala wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sharifa Lengima, alisema wamekuwa wakijitahidi kutetea haki za watumiaji wa huduma za nishati na maji.

# Bomba la mafuta lashusha neema ya maji jijini Tanga

**Na Oscar Assenga,** TANGA

ZAIDI ya wakazi 26,071 wa kata za Chongoleani, Mzizima na Mabokweni za Halmashauri ya Jiji la Tanga watapata maji kwa saa 24 kila siku baada ya kukamilika mradi unaotekelezwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA).

Akitoa taarifa kwa kiongozi wa mbio za mwenge kwa mwaka huu, Godfrey Mnzava wakati wa kuzindua mradi huo, Mhandisi wa Miradi ya Maji Tanga UWASA, Violet Kazumba, alisema ulianza kujengwa Novemba mwaka 2022 na Mkandarasi wa jijini Dar es Salaam.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2024, Godfrey Mnzava (katikati), akifungua koki ya maji baada ya kuzindua mradi wa maji katika Kata ya Chongoleani, jijini Tanga juzi, unaofanywa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga (TANGA UWASA). Kulia ni Mbunge wa Jimbo la Tanga na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na (kushoto) ni Mhandisi wa Miradi wa Tanga Uwasa, Violeth Kazumba. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

Kazumba alisema mradi huo umefadhiliwa na Taasisi ya ulazaji wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanzania.

Alisema usanifu wake unakadiriwa kugharimu kiasi cha Sh. 2,352,201,500 na hadi sasa mkandarasi amelipwa Sh.1,823,766,540 sawa na asilimia 79.46.

Alisema mradi huo ulikamilika Machi mwaka huu kwa asilimia 100 na hadi sasa unatoa huduma kwa jamii na mamlaka hiyo inaendelea kuunganisha maji kwenye matawi na watu binafsi.

Akizungumzia faida za mradi huo, Kazumba, alisema utawezesha wakazi wa kata hizo kupata huduma ya maji safi kwa saa 24 kila siku.

Awali kiongozi wa mbio hizo za Mwenge, alisema ameridhishwa na utekelezaji mradi huo.

Mnzava alisema wamekuwa wakitekeleza maelekezo ya Serikali ya kutangaza miradi yote na zabuni kwenye Mfumo wa Kidigitali wa Zabuni (NEST).

Alisema wanaendelea kusisitiza utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa fedha kutoka serikali kuu, wahisani,wadau wa maendeleo na mchango wa wananchi.

**Awali kiongozi wa mbio hizo za Mwenge, alisema ameridhishwa na utekelezaji mradi huo.**

# Adadi awafunda viongozi CCM, Serikali

**Na Steven William,** MUHEZA

MWENYEKITI wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini, Balozi Adadi Rajabu amewaomba viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na serikali wilayani hapa kushirikiana na kujenga umoja ili kuwaletea maendeleo wananchi.

Adadi alisema kipindi hiki siyo cha kufanya kampeni bali wanachotakiwa ni kujenga umoja wa kuleta maendeleo ya Muheza na wananchi wake.

Akizungumza na baadhi ya wananchi na viongozi nyumbani kwake Michungwani Muheza kushiriki chakula cha pamoja alichowaandalia alisema:

"Wananchi wana matarajio na imani kubwa sana kwa Serikali yao katika kuwaletea maendeleo kiuchumi na huduma bora za jamii, hivyo ni lazima sisi viongozi wa juu tushikamane kwa kuzungumza lugha moja, kutumia muda mwingi kutafuta njia bora za kutatua kero zao badala ya kila kiongozi kuzungumza lugha yake tofauti na mwenzake."

Adadi aliwataka viongozi hao na wananchi kumpa ushirikiano mkuu mpya wa wilaya yao, Zainabu Abdallah kuwaletea wananchi maendeleo badala ya kuendekeza malumbano na majungu yasiyo kuwa na tija.

Alisema wanamkaribisha kwa mikono miwili mkuu huyo wilayani hapa na kumtahadharisha kuwapo makini na baadhi ya watu aliwaowaita 'wana maneno mengi' ambayo watampelekea, hivyo wa kuyachuja ni yeye mwenyewe.

"Sisi sote tunajenga nyumba moja, hatuna sababu ya kugombania fito, tukumbuke lengo letu ni moja tu la kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuwaletea maendelo wananchi kwa kuhakikisha tunatimiza matarajio yao," alisisitiza Balozi Adadi.

Alifafanua kuwa msingi wa maendeleo ya Taifa lolote unajengwa katika dhana ya umoja, mshikamano, ushirikiano na mahusiano mazuri baina ya viongozi ambao ni watekelezaji wa sera na wananchi wenyewe ambao ni wanufaika wa fursa za maendeleo zinazoletwa na serikali kupitia miradi.


Alisema wanachohitaji kwa sasa ni kuwaletea maendeleo wananchi wa Muheza katika miradi ya maji, barabara, shule, afya na huduma za umeme ambazo wakati wa ubunge wake alianza nayo.

Alisema amewaita viongozi hao na wananchi na wazee nyumbani kwake kushiriki chakula hicho na kwamba watu wasije wakafikiria ni kampeni za uchaguzi kwani hiyo ni kawaida yake tangu hajaingia katika ulingo wa siasa.

Adadi alisema uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji unakaribia na kuwaomba wananchi wajitokeze kugombea hususani vijana na wanawake ili kupata viongozi bora.

Mkuu huyo wa wilaya alimshukuru Adadi kwa wosia aliompa na kuahidi kuwa atahakikisha anajenga umoja na mshikamano kwa wananchi wa Muheza ili kuleta maendeleo kama Pangani alikoshikilia wadhifa huo kabla ya kuhamishiwa Muheza.

Viongozi wengine wailioshiriki chakula hicho ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Juma Mhina.





# Kigogo abanwa mwananchi kuuziwa bwawa

## • Aamriwa kumrejeshea fedha

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAIMU Mwenyekiti wa Mtaa wa Shunu Kata ya Nyahanga Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Julius Sabuni ameamriwa kumrejeshea mwananchi Sh.550,000 baada ya kuuziwa eneo la bwawa la maji la Mtakuja kinyume na sheria.

Amri hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi wakimtuhumu kigogo huyo kuuza eneo hilo bila ya kufuata taratibu .

Marco Masanja, mkazi wa eneo hilo, alisema aliuziwa sehemu ya bwawa hilo ili kujenga makazi ya kudumu, lakini amezuiliwa kuendeleza ujenzi na wananchi kwa madai ni mali ya umma.

Alisema kabla ya kununua eneo hilo alifika katika Ofisi ya Mtaa wa Shunu na kukutana na Kaimu Mwenyekiti, Julius Sabuni kutaka kujua uhalali wa eneo hilo na kujibiwa kuwa halina tatizo na kununua kwa kiasi hicho.

"Mpaka sasa nimeshawekeza Sh.milioni 1.2 ikiwemo kununua vifaa vya ujenzi, kusawazisha eneo, gharama za ununuzi. naomba nipewa fidia ya eneo lingine au kurejeshewa gharama zangu nilizotumia ili kuondoa malalamiko hayo kwani sio kosa langu na niliaminishwa na serikali kabla ya kununua," alilalamika Masanja.

Akijibu malalamiko hao, Sabuni alisema eneo hilo liliuzwa na mama mmoja ambaye kwa sasa yuko visiwani Zanzibar.

Alisema awali eneo hilo lilidaiwa kuwa ni mali ya umma, lakini mahakama ilitamka kuwa ni mali ya familia hiyo, hivyo hakuwa na shaka ya kushiriki kwenye mauziano hayo.

Alisema yukotayari kurejesha fedha zilizotumika kununua eneo hilo na si Sh.milioni 1.2 kama inavyodaiwa na Masanja.

Sabuni alisema katika kikao walichokaa cha halmashauri ya maendeleo, walijadili na kumaliza mgogoro huo.

Akizungumzia mgogoro huo, Mboni alimtaka kaimu mwenyekiti huyo kurejesha kiasi kilichotumika kununua eneo hilo kinyume na sheria na kuwasihi viongozi kutokuwa sehemu ya migogoro ya ardhi na badala yake wawe kwenye usuluhishi kwa kuwaeleza wananchi maeneo sahihi na ya umma.

Alisema kwa mujibu wa sheria za serikali za mitaa, wenyeviti hawaruhusiwi kusimamia mauziano ya ardhi na badala yake wanatakiwa kumtambulisha mnunuzi kwa mmiliki halali wa eneo.

Mkuu huyo wa wilaya alionya kuwa hatasita kuwachukulia hatua za kinidhamu wenyekiti wa serikali za mitaa watakaobainika kuhusika kwenye uuzaji wa maeneo ya umma na ya wazi kwani wamekuwa chanzo cha migogoro ya ardhi na kuichafua serikali.



Ofisa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira Manispaa ya Shinyanga, Ezra Manjerenga (kulia), akitoa elimu ya upandaji miti kwa vitendo kwa wafanyakazi na wanafunzi wa Chuo cha Sayansi za Afya Kolandoto juzi, ambapo miti 150 ilipandwa chuoni hapo, ili kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. **PICHA:MARCO MADUHU**

# Wanawake wahamasishwa kugombea uongozi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UMOJA wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, umewataka wanawake wilayani humo kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kugombea uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu mwakani.

Wito huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa UWT wa Wilaya hiyo, Rehema Nhamanilo kwenye kongamano la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kufikisha miaka mitatu madarakani.

Rehema alisema wanawake wenye sifa wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi za uongozi kwenye chaguzi zijazo ukiwamo wa serikali za mitaa ambao unatarajiwa kufanyika mwaka huu ukifuatiwa na Uchaguzi Mkuu mwakani.

"Kama wewe Mwanamke anajifahamu una sifa ya kuwa kiongozi jitokeze uchukue fomu ya kugombea nafasi ya uongozi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao utafanyika mwaka huu, pamoja na Uchaguzi Mkuu mwakani, ili tufikie 50 kwa 50 na wanaume kwenye nafasi za uongozi," alisema.

Mgeni rasmi kwenye kongamano hilo, Katibu wa Jumuiya ya Wazazi CCM Mkoa wa Shinyanga Regina Ndulu aliwataka wanawake kuwaunga mkono, kuwapigia kura za ushindi na si kuwatolea lugha chafu za kuwakatisha tamaa wenzao watakaojitokeza kugombea nafasi mbalimbali.

Diwani wa Viti Maalum Tarafa ya Ibadakuli, Zuhura Waziri ambaye ndiye aliyeandaa kongamano hilo, alisema Rais Samia amefanya mambo makubwa kwenye uongozi wake ndani ya miaka mitatu na kila mtu ameshuhudia maendeleo makubwa nchini.

Aliwataka wanawake waendelee kupendana na kusameheana wanapokwaruzana.

**Wito huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa UWT wa Wilaya hiyo, Rehema Nhamanilo kwenye kongamano la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kufikisha miaka mitatu madarakani.**

# Kamati kuchunguza mauaji Hifadhi ya Serengeti

**Na Neema Emmanuel,** SERENGETI

SERIKALI imeunda kamati ya kuchunguza mauaji ya watu katika maeneo ya hifadhi ya wanyama ya Serengeti mkoani Mara.

Hayo yalisemwa juzi na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara Abdulrahman Kinana katika kikao cha wanachama wa chama hicho wilayani hapa baada ya kupokea malalamiko yakiwemo ya mauaji hayo.

Kinana alisema ni wakati wa viongozi kuwaelimisha wananchi kuheshimu mipaka iliyopo na kukemea mauaji ya watu yanayodaiwa kutokea mara kwa mara kwenye hifadhi hiyo.

Alisema hakuna mwenye haki ya kuondoa uhai wa mtu hata kwenye Katiba haki ya kwanza ni kuishi.

Kinana alisema serikali hairuhusu kukatishwa kwa maisha ya mwananchi yeyote, vyombo vya ulinzi na usalama wajibu wake ni kufuata sheria na kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo.

Akizungumzia kero ya mpaka kati ya Wilaya ya Serengeti na Bunda, Kinana, alisema amezungumza na Kamati ya Siasa ya Wilaya na kuelezwa limekuwepo kwa zaidi ya miaka 50.

"Nikajiuliza kwa nini liwepo wakati watu wa Bunda na Serengeti ni ndugu na kwa kuwa wazee wapo watatuongoza katika hili nitashauriana na viongozi wa Mkoa wa Mara na wa kitaifa kwa mtazamo wangu," alisema na kuongeza kuwa:

"Hili jambo ni la kijamii si la kiserikali kabla ya kutenganishwa Wilaya ya Bunda na Serengeti ilikuwa moja na inawezekana kugawa watu, lakini huwezi kugawa undugu."

Akizungumzia ubovu wa barabara inayounganisha Sanzati, Nata hadi Arusha yenye urefu wa kilometa 40, Kinana, alisema amepokea kero hiyo na kuzungumza na Waziri wa Ujenzi, Inocent Bashungwa kuhusu ujenzi wake.

Diwani wa Kata ya Machochwe, Joseph Magete alisema kuwa kumekuwepo na matukio ya kutatanisha pembezoni mwa hifadhi hiyo ya watu kupotea na kuiomba serikali kufuatilia ili kubaini kinachoendelea



Ukurasa 12

KWAKE MWALIMU PROF. KITILA...

**Ubadilishaji uzio, samani, matundu vyoo inavyobadilisha elimu Ubungo**



Ukurasa 13

Wagundua nyangumi wanavyozungumza

Nipashe

# TESA

Jumanne Aprili 16, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Ingia darasani, ulaji ukwaju kunavyokuondolea maradhi**

ELIMU

NA PETER ORWA

WADAU, WALIMU VS WAZAZI...

# Ufunguo anaotumia Rais Samia kusuka elimu kwa mahitaji ya leo

JUMANNE iliyopita mada gazetini ilijadili nafasi ya mwalimu na mwanafunzi kuwa ndio nguzo ya kwanza katika taaluma wakati wa kufanikisha elimu, mafanikio yake yakiungwa na msamiti 'ukiona vinaelea vimeundwa.'

Mafanikio ya moja kwa moja upande wa mwalimu darasani, huwa nyuma yake kuna mchango wa serikali ikimtetea. Vivyo hivyo, mwanafunzi akisimamiwa katika maeneo ya kila siku na wazazi au walezi.

Serikali inapowekeza katika kuelimisha na ajira ya wataalamu wanaoingia darasani kufundisha, ujenzi wa madarasa na mahitaji ya kitaalamu yanajibu kuboreka elimu ya anayefunzwa darasani, pia mfundishaji akitanuka kifikra.

Mwalimu ni mfanyakazi, anapaswa kuthaminiwa kwa mahitaji yote muhimu ya kimaslahi kama mshahara, posho na huduma; makazi na tiba. Anatulia kifikra na tija yake darasani inakuwa juu.

Wazazi na walezi, hao wanaangukia katika wawezeshaji wakuu 'namba moja' nje ya darasa. Mahitaji yote ya kisheria, kisera na kimila kwa mwanafunzi kama vile muda wa mwanafunzi kusoma, mahudhurio yake shule, pia kuhudumia mahitaji kama sare na madaftari.

Hiyo huenda mbali katika mahitaji mahsusi na maelekezo ya kishule, kisheria na kiserikali kama vile njia maalum za kumlinda mwanafunzi wa kike, ni jukumu lake mzazi kuanzia nyumbani na anaikabidhi shule, pale mwanafunzi anaingia ndani ya geti lake.

Wakati wote huo, nyuma ya pazia mamlaka ya kiserikali inaangalia kuhakikisha shule na wazazi hawatoki nje ya msimamo.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na wanafunzi wasichana, alipokuwa ziarani mkoani Lindi. **PICHA: MTANDAO**

### DARASA LA SAMIA

Hivi karibuni nchini ilifuatiliwa kwa kina, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa akifanya uwekezaji mkubwa kiserikali katika elimu nchini na amefanya hilo, kulingana na mahitaji ya sasa kielimu, mwendelezo wa kile ambacho watangulizi wake wamemtangulia.

Daima huwa kuna mambo makuu matatu kutoka serikali: Kuandaa sera na mitaala; kuwekeza kwenye miradi ya kielimu; pia inasimamia kuhakikisha inafanikiwa.

Hivi sasa kunashuhudiwa mabadiliko katika mfumo wa elimu shuleni.

Mitaala, inafanyiwa mabadiliko makubwa, mfano kuanzishwa kwa tahasusi (combination) mpya katika kidato cha tano shuleni, ili kuendana na mahitaji ya sasa na ndio maana masomo ya lugha mpya kama za Kiarabu na Kichina zikiwamo, pia dhana ya kompyuta.

Pia, katika maboresho hayo, utawala wa nchi katika Awamu ya Sita umebadili mtaala kwenye mabadiliko makubwa yakionekana hasa kwa madarasa ya kwanza na pili, huku elimu ya msingi kuishia darasa la sita.

Hapo ikiangaliwa kisera, mabadiliko hayo yanachukua sura sasa anayeanza darasa la kwanza, anaendelea nayo hadi kidato cha nne, tofauti na zamani kulikuwapo 'kufaulu na kufeli.'

Kimsingi hilo sio geni, ikizingatiwa nchini Tanzania Bara iko katika awamu sita zote za chama kilekile, zinadumisha dhana ya 'itikadi moja na kupokezana kijiti', tofauti inayojitokeza ni maboresho kulingana na mahitaji ya wakati.

Hata dhana ya kisera ya kupanua wigo wa elimu ya sekondari kupitia uwekezaji wa kata, serikali ilianza nayo katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Pili, chini ya Rais Ali Hassan Mwinyi mnamo Julai mwaka 1988, ilipoanzishwa Shule ya Sekondari Kisarawe, ambayo sehemu kubwa iliwekezwa na wananchi wa Maneromango iliko shule.

Lakini wazo hilo likaboreshwa na Rais Benjamin Mkapa katika Awamu ya Tatu, akibuni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES).

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA ROMANA MALLYA

KWAKE MWALIMU KITILA MKUMBO...

# Ubadilishaji uzio, samani, matundu vyoo inavyobadilisha elimu Ubungo

KATIKA kipindi cha miaka mitatu Jimbo la Ubungo limepokea jumla ya Sh. milioni 236.9, kwa mujibu wa Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ikimletea mabadiliko makubwa katika mfumo wale wa elimu

Mbunge Kitila, mzizi wa taaluma yake amesomea ualimu na talauma yake ikadumu darasani, kabla kubadili mwelekeo wa ajira alipoteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji.

Baadaye akajiunga na siasa, tayari akiwa wa wasifu wa profesa, anayewasuka walimu watarajiwa, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Sifa ya matokeo yake sasa, imekomboa shule ambazo zilikuwa hazina uzio na geti na kuchangia kuwapo kwa mwingiliano wa watu, pindi watoto wakiwa darasani.

Fedha nyingine zinatajwa kutawanywa katika miradi mbalimbali iliyoko katika kila kata jimboni humo katika sekta ya uchumi, miundombinu na masuala ya kijamii.

Pia, inatajwa fedha kutumika kukamilisha ujenzi na ukarabati wa baadhi ya vituo vya polisi. Kielimu, fedha za Mfuko wa Jimbo zimetumika kujenga uzio katika baadhi ya shule za msingi jimboni humo zikiwamo Makuburi, Kilimani, Uzuri, Mpakani, Mabibo na Mugabe, huku Shule ya Amani ikikarabatiwa na Kawawa kujengewa matundu ya vyoo.






Mbunge Kitila Mkumbo, akiwa na wanafunzi. Chini, mazingira ya Shule ya Sekondari Urafiki, ambayo ni mnufaika wa mradi husika jimboni Ubungo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Nilifanya hivyo kwa maana, kamati hii inahusisha madiwani na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

### SAUTI YA SHULENI

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Makuburi Hussein Dadi, anabainisha kuwa, uzio pamoja na geti lililowekwa limewasaidia kuondokana na mwingiliano baina ya wanajamii na shule.

"Wakati kukiwa hakuna uzio watu walikuwa wakikatiza maeneo ya shuleni muda ambao watoto wanaendelea na masomo, hivyo kuchangia kutokuwapo kwa wanafunzi.

"Kuna wananchi walikuwa wanapita muda wote. Mafundi magari walikuwa wanaleta magari mpaka kwenye eneo la shule na kusababisha kelele na kuondoa utulivu kwa wanafunzi na wakati mwingine usalama wa watoto ulikuwa mdogo," anasema Mwalimu Dadi.

Wanafunzi shuleni hapo, Anna Lutamboka na Hassan Juma, wanasema changamoto ya mwingiliano wa watu shuleni hapo ulikuwa ukiwaathiri katika masomo yao.

Katika ufafanuzi wao wanatamka, kuwapo kwa uzio na geti, kumechangia pia kupunguza utoro wa wanafunzi wakati wa masomo kwa kuwa kwa sasa ili watoke ni lazima wapiti getini.

Ni kauli inayoungwa mkono na naungwa mkono, pia wanafunzi wa Shule ya Msingi Mugabe iliyopo jimboni humo, wanafunzi Amini Jackson, Anita Richard na Jacklin John, wanaeleza kabla ya ujenzi wa uzio, walikuwa na changamoto kuibwa mabegi yao na watu wa nje, sasa wapo salama.

Mafanikio mengine anayataja katika sekta hiyo jimboni humo, ni pamoja na ununuzi wa samani za walimu zilizohusisha shule za msingi ambazo ni.

Hapo kunatajwa: Manzese (viti 18), Ukombozi (viti 18), Mianzini (viti 14) na Shule za Sekondari Mburahati (viti 16) na ya Kimara (viti na meza moja).

Shule nyingine za msingi zilizonufaika na samani ni : Golani, Golani B, Kilungule, Kimara Baruti, Millenia ya Tatu na Msewe (viti 26). Huk kuimenunuliwa vifaa; Laptop, zulia ofisi ya mwalimu mkuu, kifa acha cha kuhufadhi nyaraka, kabati na mapazia.

Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Urafiki, nao wanaatajwa kunufaika kwa kupatiwa madawati 120 yaliyoondoa changamoto yao, huku Shule ya Sekondari Mburahati, ikipatiwa madawati 93 na meza 93 za wanafunzi.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mianzini, Elizabeth Kambi, anasema kabla ya kukabidhiwa samani hizo iliwalazimu wanafunzi kuchangia viti, jambo lililowasababishia usumbufu.

"Mwalimu ukiacha kiti unakuta mwanafunzi kakibeba kaenda kukalia. Hii ilikuwa changamoto kubwa ambayo iliondoa umakini katika kazi na kutupunguzia ufanisi. Kwa sasa viti vya walimu haviingiliani na vya wanafunzi," anaibainisha Mkuu wa Shule Elizabeth.

### ANAVYONENA MBUNGE

Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo ambaye pia, ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, anasema aliamua kuunda Kamati Maalum kwa ajili ya kuratibu na kusimamia fedha za Mfuko wa Jimbo pamoja na miradi yote inayotekelezwa kwa fedha za mfuko huo.

Prof. Kitila anasema aliamua kuliacha jukumu la kuratibu fedha za mfuko wa Jimbo kwa kamati maalum ya mfuko wa jimbo ili kuweka usimamizi mzuri na mgawanyo wa fedha hizo katika kutekeleza miradi.

"Nilifanya hivyo kwa maana, kamati hii inahusisha madiwani na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

"Nilipoingia madarakani niliamua kuunda Kamati ya Mfuko wa Jimbo ili kuwapa majukumu ya usimamizi wa fedha na miradi inayotokana na mfuko huu.

"Fedha za mfuko wa Jimbo zinatolewa kwa ajili ya kuchochea maendeleo pale ambapo wananchi wanakuwa wameanzisha jambo lao tumekuwa tukiwashika mkono kwa kumalizia," akabainisha Prof. Mkumbo.

Anasema mambo mengine ya kijamii yaliyofanyika kwa lengo la kugusa maisha ya wananchi aliyataja ni pamoja na ujenzi wa vizimba vya mama lishe katika Soko la Mawasiliano, kuchochea shughuli za kiuchumi kwa vijana wa Kata ya Makuburi na shughuli za kiuchumi kwa wanawake wa Makurumla.

Jimbo la Ubungo ni miongoni mwa majimbo 10 yaliyoko mkoani Dar es Salaam likiwa katika wilaya ya Ubungo yenye majimbo mawili ya Ubungo na Kibamba.

### ULINZI NA USALAMA

Kuna mazao yanayovunwa zaidi ya lengo kuu la kuboresha elimu. Hapo Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Mavurunza, Taji Kanuti, anasema kuanza kufanya kazi kwa Kituo cha Polisi Mavurunza kumesaidia kuongeza utulivu na ulinzi katika Kata ya Kimara na maeneo jirani kutokana na kituo hicho kuwa kikubwa.

INAENDELEA UK.13

TEKNOLOJIA
NA MWANDISHI WETU

# Wagundua nyangumi wanavyozungumza

ILIKUWA mwaka 2021, nje ya pwani ya Kusini-Mashariki mwa Alaska, timu ya wanasayansi sita ilicheza rekodi ya sauti ya salamu kupitia spika iliyo chini ya maji.

Walipigwa na butwaa walipogundua nyangumi mmoja waliyemwita Twain, alipojibu sauti hiyo. “Ni ajabu,” anasema Josie Hubbard, mtaalamu wa tabia za wanyama katika Chuo Kikuu cha California, Davis ambaye nae alikuwa kwenye chombo hicho.

“Lazima uzime chombo umbali wa mita kadhaa walipo nyangumi. Katika tukio hili, Twain mwenye umri wa miaka 38 alikwenda kwenye chombo, na kukizunguka kwa dakika 20,” anasema Hubbard.

Twain alipoondoka, Hubbard akaenda chini ya chombo na ndipo wakagundua nyangumi huyo alikuwa akijibu sauti ya spika kwa dakika zote 20. Sauti ndefu inayokuja na kupotea, ikiwa na mapigo na milunzi.

Wanasayansi waliweka vifaa vya kurikodi baharini ili kukusanya sauti za nyangumi, ambaye akaonyesha orodha ndefu ya tabia zinazofanana na za wanadamu.

Wanashirikiana wenyewe na viumbe wengine, huku wakifundishana stadi za maisha, kama kutunza watoto na kucheza.

Tofauti na wanadamu, inaelezwa wanatumia zaidi sauti kuliko macho kwenye mambo yao mengi. Sauti zao zinaweza kusafiri mbali na kwa kasi ndani ya maji kuliko inavyosafiri hewani.

Nyagumi aina ya Cetaceans kwa mfano, wanaelezwa hutegemea kelele kuwasiliana wenyewe, kusafiri, kutafuta wenza na chakula, kulinda maeneo na rasilimali zao na kuepuka wanyama wanaokula wenzao.

Watoto wao wanatajwa nao hulia kama watoto wachanga wa binaadamu, wengine wanaaminika kuwa na majina na makundi yao kutoka sehemu tofauti za bahari huwasiliana lugha za eneo.



Nyangumi akiwa na mtoto wake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Wanasayansi waliweka vifaa vya kurekodi baharini ili kukusanya sauti za nyangumi.

Nyangumi husikika wakiiga lahaja za vikundi vya kigeni- na wengine wanadhaniwa kuiga sauti ya kibinadamu.

### REKODI ZAO

Rekodi ya kwanza ya nyimbo za nyangumi ilipatoka anarekodiwa mwaka 1952 na Mhandisi wa Jeshi la Wanamaji la Marekani, Frank Watlington.

Takriban miaka 20 baadaye, mwanabaiolojia wa baharini Roger Payne akagundua sauti hizo zilipangwa kwa kujirudiarudia. Hilo hubadilisha uelewa wa sauti za nyangumi na kuzua shauku iliyowapeleka miongo kadhaa ya utafiti.

### KINACHOFUATA

Watafiti wanatumai kuchambua sauti za nyangumi kunaweza kusaidia kuelewa sauti zao. Watafiti wanadhani kuwa sauti za nyangumi zina ujumbe wenye maana.

Hata hivyo, wanasema uelewa wetu wa mawasiliano ya nyangumi bado uko katika hatua ya awali sana.

Ni katika kipindi chote cha kubadilishana sauti, Twain kila mara akaitoa sauti kama iliyotoma katika spika na kila baada ya sekunde 10, naye akatoa sauti hiyo. Hiyo ilifanywa mara 36 kwa dakika 20.

“Changamoto kubwa kwetu ni kuelewa sauti hizo na kuamua maana yao, ili tuweze kujua maana. Nadhani AI itatusaidia kufanya hivyo,” anassema Brenda McCowan, Mtafiti katika timu hiyo.

Umbali wa zaidi ya kilomita8,000), kundi la wataalamu wa akili bandia, lugha asilia, waandishi, wataalamu wa lugha, wanabiolojia wa baharini, wataalamu wa roboti - wanatarajia kutumia AI - kufafanua sauti za nyangumi.

Timu hii nyingine ilizinduliwa mwaka 2020, Ceti (Cetacean Translation Initiative), ikiongozwa na mwanabiolojia wa baharini David Gruber, imekuwa ikirekodi kundi la nyangumi katika pwani ya Dominica, kisiwa cha Karibea, kwa kutumia maikrofoni kwenye maboya, samaki wa roboti na vifaa vilivyowekwa kwenye migongo ya nyangumi.

“Ni vigumu kwetu kuelewa ulimwengu wao, zaidi ya maingiliano haya mafupi sana ya sauti. Huyu ni kiumbe wa kipekee, mpole, na kuna mengi tu yanayoendelea katika maisha yake,” anasema Gruber.

“Kila wakati tunapotafiti, tunapata utata na namna mpya zaidi katika mawasiliano yao.”

Anaamini baadaye kutafikiwa hatua ya maendeleo ya kiteknolojia, kuwezesha mawasiliano naa nyangumi.

Hadi sasa, taarifa zilizokusanywa zinafanyiwa uchambuzi kwa kutumia mashine, kugundua maana ya sauti hizo, na matokeo yanatarajiwa kutolewa mwaka 2024. Samantha Blakeman, Meneja wa Data za Baharini wa Kituo cha Kitaifa cha Oceanography, ana ufafanuzi: “AI inaweza kuturuhusu kuelewa mifumo ya mawasiliano ya viumbe vingine vingi.

“Nadhani litakuwa jambo zuri kwa ulimwengu - ikiwa tunajali kuhusu kile ambacho nyangumi wanasema.”

***• Kwa mujibu wa habari za mtandaoni kimataifa.***

## Ubadilishaji uzio, samani, matundu vyoo inavyobadilisha elimu Ubungo

**INATOKA UK.12**

“Kilichukua muda mrefu kujengwa, lakini kwa awamu yake kwa kutumia fedha za mfuko wa jimbo, fedha zake binafsi pamoja na wadau wengine kimekamilika,” anasema Kanuti.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Sophia Fitina, anasema kuwapo wa Kituo cha Polisi Kibo, ni msaada mkubwa kwa wakazi wa eneo hilo na utasaidia kupunguza vitendo vya uhalifu kwa kuwa, awali walikuwa wakifuata huduma za polisi katika Kituo cha Polisi Kimara Mwisho, ambako ni mbali na mtaa wao.

Diwani wa Kata ya Kimara, Ismail Mvungi, amepongeza kazi kubwa iliyofanyika na kutaka wananchi kulinda miundombinu iliyotengenezwa kwa kuifanyia ukarabati pale inapoharibika.

“Hii miradi imeshakabidhiwa kwetu hatuna budi kuitunza na kuifanyia matengenezo ya mara kwa mara ili idumu na kuendelea kutusaidia,” anasema.

Diwani wa Kata ya Makuburi, Olver Shirima, anasema katika eneo lake kumejengwa vivuko viwili cha Mikongeni na Uluguruni ambavyo vimesaidia wananchi kuondokana na adha waliyokuwa wakiipata awali.

Anna Esau, Amina Hamis na Mjuni Mjunwa ni wakazi wa Kata Makuburi ambao wanaeleza kuwa, kivuko cha Mikongeni na kile cha Uluguruni vimeondoa changamoto kwao, kwani wakati wa mvua walishindwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine kutokana na kutatika kwa mawasiliano.

Diwani wa Kata Sinza, Raphael Awino, anaeleza kuwa Mtaa wa Nungunungu Sinza E, umejengewa mtaro na kivuko cha waenda kwa miguu pamoja na ujenzi wa barabara ya Sinza E na B ukiwa katika hatua za awali.

Sekta nyingine ambazo zimeguswa ni ukarabati zikiwamo Ofisi za Mitaa ya Uzuri na Kilimani Kata ya Manzese, Ofisi ya Mtaa wa Jutegemee, Kata ya Mabibo, Ofisi ya Mtaa wa Kimamba, Kata ya Makurumla na Ofisi ya Mtaa wa Kisiwani, Kata ya Mburahati.

Pia, kumefanyika ujenzi wa vivuko katika maeneo mbalimbali hasa yale ambayo yaliyokuwa na changamoto ya mawasiliano kipindi cha mvua.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ingia darasani, ulaji ukwaju kunavyokuondolea maradhi

UKWAJU unajulikana zaidi kwa matumizi yake katika vyakula hasa katika maeneo ya bara Asia, Amerika Kusini, visiwa vya Caribbean na Afrika. Hata nchini Tanzania, si haba ukwaju una nafasi yake, wengi katika jamii wamekulia na wanaendeleza mlio wake.

Lakini huenda wengi wamedumu katika utamu wa uchachu wake, iwe moja kwa moja au ikiungwa juisi au uji na wasijue zaidi ya hapo, mbali na dhana 'hayo ni matunda'

Ukweli ni kwamba vilevile ukwaju huo, ni maarufu katika uponyaji maradhi mbalimbali. Mtu akipatwa na maumivu, ukwaju unatumika kupunguza maumivu, kutuliza usumbufu wa tumbo na kutuliza homa.

Watafiti wa zama hizi wamegundua kuwa ukwaju unaweza kutoa faida zaidi za kiafya kuliko ilivyokuwa inajulikana hapo awali.

Katika dawa za jadi, ukwaju umetumika kutibu matatizo yanayohusiana na ini. Ulaji wa ukwaju pia hutumika kutuliza kichefuchefu.

• Ukwaju huo, pia unatuliza kinga ya mwili kwa kuzalisha virutubisho vinavyoitwa 'procyanidins; wataalamu wakiamini vinalinda ini na kukabiliana na magonjwa ya ini.

Kama ilivyo kwa matunda mengi ya rangi nyeusi, ukwaju nao una virutubisho vingi viitwavyo kitaalamu 'polyphenols' na vingine 'flavonoids. Hivyo hurekebisha viwango vya mafuta mwilini



Tunda ukwaju katika mandhari tofauti. **PICHA: MTANDAO**

Mtu anapotumia ukwaju, kuna uwezekanio wa kusaidiwa katika kuvunjika na kupunguza mafuta katika damu. Hiyo inasawazisha viwango vya mafuta kunaweza kusaidia afya ya moyo na mishipa kwa ujumla.

• Eneo lingine ni pale ukwaju unapambana na maradhi ya saratani; Virutubisho vya ukwaju vinatajwa kuzuia uharibifu wa seli hizo. Vinakabiliana na athari za molekyuli mwilini, ambazo zinahusishwa na mabadiliko ya seli hata kusababisha mtu kuugua saratani.



Ukwaju hutoa kinga nyingi kwa mwili. Katika utafiti kwa wanyama, watafiti waligundua virutubisho vya ukwaju vinapunguza uharibifu unaosababishwa na saratani ya seli za figo.

• Kupambana na maambukizi; Ukwaju hutumika kuondoa maambukizi, ikitumiwa kama dawa ya kutuliza maumivu ya majeraha, ukwaju unaweza kupunguza uvimbe na maumivu kwenye jeraha.

Watafiti wamegundua unaweza kupunguza uvimbe wa ndani, huku ukipambana na maambukizi mpya.

• Kupambana na kisukari; Ukwaju una virutubisho vinavyoboresha udhibiti wa sukari ya damu kwa wale walio na ugonjwa wa kisukari.

Ukwaju unatumika kama msaada wa lishe na kuunganishwa na dawa za ugonjwa wa kisukari na hurekebisha tishu zilizoharibika.

• Kinga na tiba Ngozi; matumizi ya ukwaju yanaweza kuwa na faida kwa matatizo ya ngozi, majipu, na shida zingine za ngozi.

Virutubisho vilivyopo katika ukwaju hutoa kinga kwa mwili na huonyesha ulinzi dhidi ya uharibifu wa ngozi kutokana na mionzi ya jua.

Kama chakula, ukwaju ni familia ya kunde na hivyo una uwezo wa kusababisha athari ya mzio kwa baadhi ya watu.

Ukwaju unaweza kupunguza viwango vya sukari ya damu na kwa hivyo unapaswa kutumiwa kwa tahadhari ikiwa una ugonjwa wa kisukari. Unaweza pia kusababisha kuharisha ikiwa utatumiwa kwa kiasi kikubwa.

***• Kwa mujibu wa taarifa kimataifa***

## Ufunguo anaotumia Rais Samia kusuka elimu kwa mahitaji ya leo

**INATOKA UK.11**

Ni mkakati wa MMES uliosambza mno shule za sekondari kama ubunifu wa Maneromango, mwaka 1988, huku anayefuatia, Jakaya Kikwete katika Awamu ya Sita, akafanya maboresho makubwa ya alichoanzisha Mkapa.

Hapo nchini kukaneemeshwa ajira kwa walimu wengi kupunguza pengo la awali, kukitanuliwa ajira ya walimu iliyopunguza pengo la awali, walilotumia kutanua usaili wao katika vyuo vikuu nchini, hata kupata wahitimu wengi. Hiyo haikushangaza, pale mwanamama Dk. Samia akapokea kijiti akiona pengo mojawapo akifanyia uwekezaji mkubwa.

Hilo ni la mabinti kuwatunulia wigo wa nafasi ya kuendelea kielimu, sasa nchini kuna mradi wa mabilioni kuwa na sekondari za mabweni mahsusi kwa wasichana, huku akiwakinga kisera hata wanaopata mimba, kuendelea na masomo.

Mzazi mara zote anaendelea kuwa sehemu ya nyenzo za mabadiliko tajwa, kwa kuwa ndio mfanikishaji mkubwa.

### NAFASI YA WADAU

Wadau katika elimu ni wengi kimsingi, kwa kuwa kila mtu ana mahitaji ya elimu, iwe rasmi au isiyo rasmi na 'elimu haina mwisho.'

Elimu na wataalamu wa elimu huzalishwa na ndio maana haishangazi katika vyuo vikuu vyote duniani havikosi vitivo au shule za elimu.

Hao ndio wanakuwa katika sura moja wanaiangalia elimu nchini inavyoenda, wakishauri, kushirikiana nao, kuisifu na hata kuikosoa serikali inavyoendesha elimu, lengo ni kusonga kuelekea kwenye ubora.

Huko nyuma, hata katika historia ya maboresho ya kuwa na sekondari ya kata nchini, inaanzia kwa walimu na Waziri mstaafu, akaishauri serikali akiwa nje ya Baraza la Mawaziri, ikapokewa kwa mafanikio ya MMES, ambayo leo shule hizo ndio nguzo za taifa.

Pia, wadau hao katika vyuo ngazi zote, ndio wanaonoa wataalamu hata kufanikisha mazao bora za kuzalisha wanafunzi bora shuleni. Mfano, Mzee Jackson Makweta, ni Waziri wa Elimu, pia Mkuu wa Shule nje ya Baraza la Mawaziri, ndiye aliibua wazo la kutanua sekondari za kata katika awamu ya tatu.

### ELIMU NI MTAJI

Hata inaporejewa historia ya nchi, hatua ya kwanza iliyofanywa na Mwalimu Nyerere katika miaka mitatu ya uhuru kukiwa hakuna sera ya muda mrefu, mwaka 1961 baada ya uhuru akatangaza elimu kwa wote shuleni, akiondoa mfumo wa kitabaka.

Pili, elimu nchini ikatengenezewa mwelekeo kisera, ikichukua sura tatu kuu; Elimu ya Shule Msingi, Elimu ya Vyuo na Elimu ya Watu Wazima.

Hata mwaka 1964, Mwalimu Nyerere katika Mpango wa wa miaka Mitano ya Uhuru 1964 – 1969, ukiwa ndio wa kwanza, uwekezaji mkubwa ulikuwa katika elimu ya msingi, lengo kutanua wigo kufikia wanafunzi wengi.

Ni dhamana hiyo ikafika mwaka 1976, serikali ikafika hatua tena serikali ikabeba dhamana yake kuandaa mtaala mpya wa elimu, ambao ukadumu muda mrefu, ukiendana na sera ilivyo, masomo kama elimu ya siasa.

Ndio sasa, maboresho yanayoshuhudiwa kutanua wigo wa madarasa mahsusi kwa mabinti sekondari, huku mitaala ikiandaliwa mageuzi yaliyoanza kutumika Januari mwaka huu.





# Kisukari, presha bado tishio nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Msaidizi Elimu ya Afya kwa Umma wa Wizara ya Afya, Dk. Tumaini Haonga amesema katika kipindi cha miaka 10 Tanzania imekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kutokana na mtindo wa maisha na watu kutofanya mazoezi.

Dk. Haonga alibainisha hayo juzi jijini hapa baada ya matembezi ya hisani ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya Afya Duniani yaliyojumuisha wafanyakazi wa wizara hiyo na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Alisema miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko kubwa la wagonjwa wa magonjwa hayo nchini yanayosababishwa na mtindo wa maisha.

"Katika miaka takribani 10 sasa Tanzania imekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kutokana tabia bwete za kutofanya mazoezi na ulaji wa vyakula usiyozingatia lishe bora" alisema Dk.Haonga

Alimtaka kila mwananchi kuchukua hatua ya kukabiliana na magonjwa hayo kuacha tabia bwete na kufanya mazoezi.

"Wananchi wenzangu muhimu kila mmoja wetu kuchukua hatua kukabiliana na magonjwa haya ambayo yalikuwa siyo tishio sasa ni Tishomingo zamani malaria ilikuwa inasumbua lakini hivi sasa ni magonjwa yasiyo ya kuambukiza, " alisema.

Dk. Haonga, alisema pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa serikali katika sekta ya afya ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya, hopitali bado gharama kubwa za matibabu kwa wanachi ni kikwazo.

"Ndiyo maana leo hii serikali yetu imesaini sheria ya huduma ya bima ya afya kwa wote ili kuwezehsa wanachi wake kupata huduma za afya zenye ubora na za uhakika kila wanapohitaji, "alisema

Mmoja wa washiriki wa matembezi hayo, Magdalena Hoya, alisema wanalishukuru WHO Ckwa kuratibu matembezi hayo ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya Afya Duniani.

Magdalena, alisema ipo haja kwa Watanzania kujenga tabia ya kufanya mazoezi kwa ajili ya kulinda afya na kujikinga na magonjwa hayo ikiwemo kisukari na shinikizo la damu.

## Wajawazito wahimizwa kujifungua vituo vya afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida imewataka wajawazito kwenda kujifungua kwenye vituo vya afya ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Mwenyekiti wake, Bertha Nakomolwa alitoa rai hiyo wilayani Mkalama katika ziara ya Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya hiyo na kukagua Kituo cha Afya cha Kata ya Gumanga baada ya kuanza kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Bertha, alisema serikali imejenga hospitali, vituo vya afya na zahanati nyingi karibu kila kata, hivyo hakuna sababu kwa wajawazito kujifungulia nyumbani wakati vituo cha afya vipo, vifaa na wahudumu wazuri.

Alisema kujifungulia nyumbani ni hatari kwa mama na mtoto hasa pale itakapotokea changamoto, hali inayoweza kusababishia vifo.

Mwenyekiti huyo aliishukuru Serikali kwa kujenga kituo hicho kwa kuwa kimesaidia kuondoa changamoto ya wananchi kutembea umbali mrefu kufuata hudumu za matibabu.

Wajumbe wa kamati hiyo waliishukuru serikali kwa kusogeza huduma za karibu na wananchi kwa kujenga kituo hicho.

Kamati hiyo imeendelea na ziara yake ya kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa kupitia Ilani ya CCM na kufanya mikutano ya hadhara na wananchi katika wilaya zote mkoani Singida



Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamagamba Kabudi (kushoto), akifurahia jambo na Mbunge wa Kwimba, Shanif Mansoor walipokutana katika viwanja vya Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Polisi waja na kampeni ya haina mhalifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma limezindua kampeni ya 'familia yangu haina mhalifu 2024' kwa shule za msingi ili kutokomeza uhalifu nchini.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika Shule ya Msingi Chadulu, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Theopista Mallya, alisema wameamua kuanzia shule za msingi kwa kuwa wanaamini watoto wadogo wakipewa elimu ni rahisi kufanyia kazi.

"Hatuishii hapa tutakwenda kwenye nyumba za ibada ili kuwapa watu elimu kuhakikisha kama familia hazitakuwa na uhalifu basi mtaani hakutakuwa na uhalifu," alisema Kamanda Mallya.

Alisema jeshi hilo limejipanga kutoa elimu kukabiliana na uhalifu kwenye familia.

"Kuna baadhi ya familia uhalifu unatendeka ndani na kama familia ipo kwenye mtaa basi kutakuwa hakuna amani wala usalama kwa sababu hiyo familia itakuwa inasumbua mtaa, kuwatumia watoto wadogo watatuambia kama kwenye familia yao kuna wezi, wabakaji, walawiti na vipigo," alisema.

Aliwataka watoto kuhakikisha familia zao hakuna uhalifu.

"Tutapambana na hao maharamia wanaolawiti na kubaka watoto, na niwaambie watu wa Dodoma nitaendelea kutoa elimu kwa makundi yote kinachotakiwa ni ushirikiano na Jeshi la Polisi ili kutokomeza uhalifu Dodoma," alisema.

Kamanda huyo, alisema ushirikiano kati ya jamii na jeshi hilo utasaidia kutokomeza vitendo hivyo katika jamii.

"Watoe taarifa za uhalifu tutawalinda simu ipo wazi saa 24 piga mwananchi yeyote tutafanyia kazi taarifa zako, na usimsingizie mtu tukikubaini tutakuchukulia hatua," alionya.





# Mafuriko yaharibu miundombinu ya maji

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

BAADHI ya maeneo ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya yamekumbwa na uhaba wa maji ya bomba baada ya miundombinu kuharibiwa na mafuriko ya mvua zinazoendelea kunyesha.

Maeneo hayo ni Nzovwe, Iyunga, Viwandani, Inyala, Ikuti, Iwambi, Itende, TAZARA, Kalobe na Sistila ambayo yanategemea maji kutoka chanzo cha Haji Halewa kilichopo Kata ya Swaya na Iyela.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), Gilbert Kayange, alisema miundombinu ya vyanzo hivyo imeng'olewa na mafuriko hayo na kubomoa baadhi.

Kayange, alisem sababu nyingine ni uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya ukanda wa juu na kupunguza kiwango cha uzalishaji wa maji kwa asilimia 20.

"Menejimenti nzima ya mamlaka inaendelea na jitihada za usiku na mchana ili kuhakikisha vyanzo hivi vinarejea katika hali yake ya kawaida na wananchi wanaanza kupata huduma, chanzo cha Iyela tayari tumekamilisha na huduma imerejea kwa wananchi," alisema Kayange.

Alisema wananchi wameharibu vyanzo vya maji kwa kuendesha shughuli za kilimo kwenye kingo za vyanzo vya maji na kuiongezea mamlaka gharama za uendeshaji kutokana na kulazimika kutumia dawa nyingi kuyatibu maji hayo.

Baadhi ya wananchi walisema kutokana na tatizo hilo wanalazimika kwenda kutafuta maji umbali mrefu na baadhi kutumia ya kwenye visima ambayo si salama kwa afya zao.

Zainab Mboya, Mkazi wa Kata ya Nzovwe, alisema mvua ikinyesha wanakinga maji na kuyatumia, lasivyo wanatumia muda mwingi kwenda kutafuta maeneo mengine yanakopatikana.

"Kama unavyoona hapa tuna bomba lakini maji hayatoki, hatuwalaumu mamlaka ya maji kwa sababu mafuriko hawajasababisha wao ila tunawaomba watumie mbinu zao kuturejeshea huduma," alisema Zainab.

Michael Sumbi, Mkazi wa Kata ya Iyunga, alisema wanahofu ya kuibuka magonjwa ya mlipuko kutokana na maji wanayotumia baada ya kukatika yanayozalishwa na mamlaka hiyo.

Alisema baadhi yao wanachota maji ya kwenye chemchem ambazo zinavamiwa na mafuriko na kuna hatari wakakumbwa na kipindupindu.

Mafuriko yanayosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha mkoani Mbeya pia yamesababisha kukatika kwa mawasiliano ya barabara kwenye baadhi ya maeneo.



Baadhi ya wakazi wa Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya, wakiangalia lori la mizigo lililoshindwa kupanda mlima Iwambi na kuanguka pembezoni mwa barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM), mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vijiji kujengewa barabara ya changarawe

**Na Nebart Msokwa,** MOMBA

WAKAZI wa vijiji vya Mfuto na Machindo vilivyopo Kata ya Myunga Halmashauri ya Momba mkoani Songwe wanatarajia kuondokana na adha ya kukosa mawasiliano baada ya serikali kutenga Sh. Milioni 135 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe.

Wakazi wa vijiji hivyo ambao kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 zaidi ya 10,000 wamekuwa wakikosa huduma muhimu ambazo katika makao makuu ya kata hiyo ikiwemo afya na kuzorotesha maendeleo.

Ujenzi wa barabara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Victor Seif alipofanya ziara wilayani Momba Septemba mwaka jana.

Akizungumza kwenye mikutano wa hadhara ya vijiji hivyo, Mbunge wa Momba, Cndester Sichalwe alisema katika ziara hiyo walimuomba mtendaji mkuu huyo kuwaboreshea miundombinu ya barabara ili kuwapunguzia wananchi kero.

Sichalwe, alisema fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo na baadaye wataendeleza kwenye maeneo mengine yakiwemo madaraja ili kuhakikisha yanapitika na wananchi wanaendelea na shughuli zao za maendeleo bila vikwazo.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kutokana na kuwa kiunganishi cha wakazi wa vijiji hivyo na makao makuu ya kata ambako zinapatikana huduma muhimu.

"Lakini kama mnakumbuka vizuri alipokuja mtendaji mkuu alituachia fedha tukaanza ujenzi wa daraja imara na la kisasa, lakini niwaambie hivi ninavyozungumza tumepata fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara yetu na muda wowote kazi itaanza," alisema Condester.

Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Momba, Francis Ngatunga, alisema fedha hizo zitatumika kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe, madaraja madogo na makaravati ili ipitike muda wote.

Alisema kwa sasa wanaendelea na taratibu za kumpata mkandarasi atakayejenga barabara hiyo ili aanze kazi mara moja na kukamilika kabla ya msimu ujao wa mvua kuanza.

Diwani wa Myunga, Yuda Mpangwe, alisema kujengwa kwa barabara katika vijiji hivyo kutasaidia kuongeza fursa za kiuchumi kwa wakulima wa mazao ya chakula na biashara.

Mpangwe, alisema wakulima hao walikuwa wanasafirisha mazao hayo kutoka mashambani kwenda nyumbani na sokoni kwa kujitwisha kichwani badala ya kutumia pikipiki na magari hali ambayo alidai ilikuwa inapunguza ufanisi.

"Tunaishukuru serikali kwa uamuzi wake wa kutujengea barabara hii, wananchi wangu wamekuwa wakipata shida hasa kipindi cha masika barabara huwa inafunga kabisa kutokana na mafuriko, hakuna gari wala pikipiki kupita," alisema Mpangwe.

Alisema wanawake wamekuwa wakipata shida kutokana na ubovu wa barabara hiyo kwa kushindwa kuvuka kwenda kliniki.

Baadhi ya wananchi waliishukuru serikali kwa kuamua kuwaboreshea barabara hiyo kwa kuwa itasaidia kuboresha huduma za kijamii.

Sabina Simfukwe, alisema kipindi cha mvua wanashindwa kusafiri na wakati mwingine wanatumia gharama kubwa ikilinganishwa na maeneo mengine ya wilaya yao.

Alisema baadhi ya wajawazito walikuwa wanajifungulia njiani wanapopelekwa kwenye Zahanati ya Myunga pekee kwenye kata hiyo.

## 'Wamiliki, madereva pikipiki, bajaji jisajilini'

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

CHAMA cha Madereva na Wamiliki wa pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji) jijini hapa kimewataka madereva na wamiliki kujisajili katika chama hicho ili kuwa na taarifa zitakazosaidia kupunguza matukio ya uhalifu na ajali za barabarani.

Katibu wa Chama hicho, Issa Mwanaluhemeja alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wandishi wa habari kuhusu matukio ya uhalifu ambayo yamekuwa yakihusishwa na vyombo hivyo jijini hapa.

Mwanaluhemeja alisema kuwa ajali nyingi zimekuwa zikitokea zikihusisha bajaji na vyombo vingine pamoja na matukio ya uporaji yakiwahusisha madereva hao.

Alisema ili kupunguza mtatizo hayo, wameamua kuanza kuwasajili madereva na wamiliki ili kuwa na taarifa kamili za kila mhusika na linapotokea tatizo wafahamu mahali pa kuanzia.

Alisema mpaka sasa wamesajili wanachama zaidi ya 3,700 na wanaendelea na kwamba yeyote ambaye hatasajiliwa atachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kuzuiwa kuendesha vyombo hivyo.

"Pamoja na kuwasajili, tunahakiki leseni za madereva ili kuhakikisha kila anayeendesha ana sifa za udereva. Ajali zinapotokea tukifuatilia tunabaini dereva hajapata mafunzo ya udereva na hana leseni hali ambayo inatuchafua wote," alisema Mwanaluhemeja.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Bajaji, Lucas Mwakyusa, alisema uhakiki wanaoufanya ni sehemu ya maboresho ya sekta hiyo hasa kuhakikisha madereva ni wale wenye sifa.

Alisema katika uchunguzi wao wamebaini kuwa baadhi ya watu walikuwa wanaendesha bajaji sio madereva ni wakabaji na waporaji wa mali za abiria.



# Mwinyi kufungua mkutano wa wakaguzi hesabu za serikali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein anatarajia kufungua mkutano wa nchi wanachama 16 za Kusini mwa Jangwa la Sahara zinazotengeneza kamati za kuchunguza hesabu za serikali kesho.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi visiwani hapa, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar, Dk. Othman Abbas Ali, alisema kufanyika kwa mkutano huo kwa mara ya kwanza Zanzibar ni fursa nzuri ya kupiga hatua mbele za maendeleo.

Dk. Ali alisema mkutano huo wenye kauli mbiu kujenga uwezo wa kamati za kuchunguza hesabu za serikali, utajumuisha wabunge kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kamati za Hesabu za Serikali (PAC) na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wa kamati hiyo.

Alisema mkutano huo utajadili udhibiti wa rushwa na uwajibikaji, uwazi kwenye sekta za maliasili katika rasilimali zisizorejesha kwa wajumbe wa PAC na kamati zinazofanana katika utekelezaji wa kazi hizo.

Alisema maofisa na wasaidizi wa PAC wakiwamo masuuli watapata fursa ya kuelezea namna fedha za umma zinatumika sahihi bila ya kuwepo viashiria vya rushwa vitakavyopelekea kupotea fedha hizo.

"Tunategemea kupata washiriki kutoka nchi zote 16 na wengine waalikwa wakiwemo wataalamu kutoka vyuo vikuu, asasi za kiraia na wakaguzi wakuu wa hesabu za serikali wakiwemo wa Tanzania, Uganda na Afrika Kusini, " alisema.

Alisema madhumuni ya mkutano huo ni kuimarisha uwezo wa wajumbe wa kuchunguza hesabu za serikali na kamati zinazofanana katika kusimamia rasilimali za fedha za umma ili kutekeleza kazi zao vizuri.

Hata hivyo, alisema matarajio ya mkutano huo ni kuangalia kanuni za msingi zinazosimamia kazi za kamati ya kuchunguza hesabu za serikali na majukumu ya kamati hizo kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

"Unayempa elimu anakwenda kufanya kazi akiwa na uwelewa wa lile analokwenda kusimamia na kutekeleza lile ambalo anafahamu, " alisema.

Alisema baada ya washiriki wa mkutano huo kujengewa uwezo watakuwa na uelewa wa kukagaua rasilimali za viwanda ambako serikali inawekeza na kuishauri namna ya kurejesha rasilimali zilizoharibika.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa anatarajiwa kufunga mkutano huo kesho kutwa.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel John Nchimbi, akimfariji Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa CCM Mkoa wa Rukwa, Auerelia Kanyengele baada ya kufiwa na mtoto wake, alipomtembelea nyumbani kwake wakati wa ziara yake ya siku mbili mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Jamii idhibiti vifo maradhi yasiyoambukiza'

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wadhamini wa Maradhi yasiyoambukiza (ZNCDs), Dk. Said Gharib Bilali amesema jamii inatakiwa kupewa elimu ya kukabiliana na maradhi ili kudhibiti vifo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi wa awamu ya pili wa kukinga na kudhibiti maradhi hayo uliofanyika Mpendae Wilaya ya Mjini Unguja, Dk. Bilali alisema kuwa

ni vema jamii kupatiwa elimu dhidi ya maradhi hayo, vichocheo na athari zake.

Alisema elimu dhidi ya maradhi hayo itaisaidia jamii kujikinga na kuweka utaratibu wa kuchunguza afya mara kwa mara na kukabiliana na ongezeko la wagonjwa.

Dk. Bilali alisema ushirikiano wa wadau na Serikali utaongeza juhudi ya kupambana na changamoto ya maradhi hayo.

Meneja wa ZNCDs Zanzibar, Haji Khamis Fundi, alisema lengo la mradi huo ni kuhamasisha jamii kufuata maelekezo ya wataalamu ili kupunguza vifo.

"Jamii ikipewa uelewa wa kutumia mfumo bora wa ulaji, kufanya mazoezi, kuacha kutumia vilevi, sigara na tumbaku, kupima afya kutasaidia kupunguza ongezeko la vifo, " alisema.

Wanachama wa jumuiya hiyo walitaja changamoto wanazokumbana nazo kuwa ni pamoja na kukosa huduma katika vituo vya afya jirani na maeneo wanayoishi na uhaba wa wahudumu wa magonjwa hayo.

ZNCDs ni mkusanyiko wa jumuiya za nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania, UgandanaZanzibarwenyelengola kupunguza vifo vitokanavyo na magonjwa hayo katika nchi zao.

# Wapendekeza marekebisho sheria za habari Z'bar

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

KAMATI ya wataalamu wa masuala ya habari Zanzibar (ZAMECO) imetoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria za habari ikiwemo ya Utangazaji namba saba ya mwaka 1997.

Ni baada ya Sheria hiyo kufanyiwa marekebisho na sheria namba moja ya mwaka 2010 kwa lengo la kupata sheria mpya na rafiki kwa waandishi wa habari na vyombo vya habari nchini.

Akizungumza katika kikao cha pamoja kati ya kamati hiyo na Tume ya kurekebisha sheria visiwani hapa, mjumbe wake ambaye pia ni Mratibu wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) Zanzibar, Shifaa Said alisema kuwa hatua hiyo ni kuhakikisha mchakato wa kupata rasimu ya sheria ya utangazaji na sheria mpya itayokidhi vigezo vya habari.

Mwandishi wa habari mkongwe, Salim Said, alisema vyombo vya habari havina nia mbaya na serikali bali ni washirika muhimu kuleta maendeleo kwa jamii.

Salim alisema jitihada za ZAMECO na wengine katika kuendeleza maboresho ya Sheria ya Utangazaji ni sehemu ya ushirikiano mzuri kati ya vyombo vya habari na serikali.

"Vyombo vya habari havina uadui na serikali, sisi ni washirika wazuri na wenye lengo jema kwa jamii na nchi kwa kuzingatia vyombo vya habari ni nguzo ya maendeleo ya uchumi," alisema Salim.

Katibu Tume ya Kurekebisha Sheria, Mussa Kombo Bakari, aliwapongeza ZAMECO kwa kutafuta maendeleo ya tasnia ya habari na kubainisha kuwa mapendekezo waliyowasilisha yamepokelewa na kufanyiwa kazi.

"Tume imekwishapeleka mapendekezo hayo katika mamlaka husika na tunatumaini yatachukuliwa kwa uzito unaostahili hatimaye rasimu ya mswaada wa sheria hiyo ipatikane," alisema Mussa.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania Zanzibar (TAMWA ZNZ), Dk. Mzuri Issa alipongeza ushirikiano kutoka kwa katibu na wafanyakazi wa tume hiyo katika mchakato huo wa kupata sheria mpya .

Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano huo katika kuhakikisha upatikanaji wa sheria mpya kwa maslahi ya Zanzibar na Wazanzibar.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**ROBI LUCIA MWITA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma : cheti cha ualimu daraja iii A chenye namba ya usajili **E0605-0036** kilichotolewa na chuo cha NG'WANZA mwaka 2016 na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **EQ2021003087** kilichotolewa na NYAROHA GIRLS SECONDARY SCHOOL – KENYA mwaka 2005. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:**PHQ/DAR.ILA/61356/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOFREY ELIAS GYUNDA**

Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4288/0047** KILICOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA Taifa kupitia ULOWA SECONDARY SCHOOL mwaka 2017.Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:**MAS/RB/325/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MTUMWA RAMADHANI NGULANGWA** anatangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba TAE655119 iliyotolewa uhamijia makao makuu .kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:**PHQ/DAR/KIN/62293/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ELIZABETH SARTHO ELIAS** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE380600** ambayo imetolewa uhamiaji makao makuu. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **9910840797669**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOHAMED TWAIBU TWAIBU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA SITA CHENYE INDEX NAMBA **S2299-0508** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA SHULE YA KITWIRU SEKONDARI MWAKA 2020.KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**YAH: MAOMBI YA URAIA WA TANZANIA**



Hii ni taarifa kwamba **ALBERT MUKENDI** MAYOMBO Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi . utaifa wake kwa sasa ni CONGO shughuli zake kwa sasa ni BIASHARA Anuani ya muajiri/ Biashara S.L.P 8602 yupo hapa nchini tangu mwaka 2007 pamoja na Mkoani Dar es salaam pia amewahi kuishi mkoani **HAKUWAHI KUISHI MKOA MWINGINE.**
Kwa yeyote mwenye sababu/ taarifa kwanini muombaji asipewe uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandashi kwa kamishna jenerali ya Uhamiaji, makao makuu ya uhamiaji, 4 Barabara ya Mwangosi , S.L.P 1181 DODOMA

AFISA UHAMIAJI (W) KIGAMBONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakam ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 437/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU PRADEEP LAXMAN PREMJI**
**WA…………………………**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA SURAJ PRADEEEP CHUDASAMA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 mwezi 05 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 03 mwaka 2024

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**MOROGORO SUB REGISTRY**
**AT MOROGORO**

**TAXATION CAUSE NO. 1923 OF 2024**
**BETWEEN**
**NDESHUKURWA ABEL SUMARI…………………APPLICANT**

**VERSUS**

**CYREKA EAST AFRICA DEVELOPMENT CO LTD…….RESPONDENT**

**NOTICE OF MENTION**
**SUBSTITUTED SERVICE**

**[Made under order V rule 16 of the Civil procedure code, cap.33 R:E 2019]**

**TO:**
**CYREKA EAST AFRICA DEVELOPMENT CO LTD……RESPONDENT**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on 17th day of APRIL 2024 at 09:30 A.M Before Hon F.Y. MBELWA, DR in the High Court of Tanzania at Morogoro.

Your required to appear in person or through your Advocate or agents dully authorized to appear on your behalf.
TAKE FURTHER NOTICE THAT in default of your appearance on that day and time the court may proceed with the application for mention in your absence.
GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 4th day of APRIL 2024.

DEPUTY REGISTRAR
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 515/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU WAHID ABEID AWADH WA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARIAM WAHID AWADH**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 08 mwezi 05 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 04 mwaka 2024

HAKIMU

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 60 LA 2024.**

**RAJABU IDD KIKOTI…………MUOMBAJI.**

**DHIDI YA**

**ACCESS BANK TANZANIA LIMITED NA WENZAKE 5…………..WADAIWA.**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**1.VENCESLAUS BONIFACE MLEKE**
**2.TIME MIRACLE LTD**
**3.KOTI BROTHERS COMPANY LTD ……..POPOTE ULIPO.**

RAJABU IDD KIKOTI amefungua shauri mbele ya Baraza la Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 16/04/2024 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza hili bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili hii leo tarehe 15 mwezi 04, 2024.

MWENYEKITI

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# ACT- Wazalendo yalia na serikali tatu

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema katika kuelekea sherehe za miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, kinataka muundo wa serikali tatu ili serikali ya Mapinduzi Zanzibar iwe na mamlaka kamili.

Kauli hiyo ilitolewa jana Dar es Salaam na Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mahusiano ya Umma wa chama hicho, Shangwe Ayo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tunatambua kwamba kilio cha Wazanzibar ni kuwa na mamlaka kamili. Na sisi ACT-Wazalendo tutakuwa sehemu ya kuhakikisha Wazanzibar wanapata mamlaka hayo kamili," alisema Shangwe.

"Kinachohitajika ili kukamilisha yote haya Katiba mpya inahitajika na tumepiga kelele kuhitaji...na tunaihitaji tangu jana na si leo tu...hii ndio itatupatia muundo wa serikali tatu, serikali ya Tanganyika na serikali kamili ya Zanzibar halafu kwenye Muungano ndio tutafute serikali ya kutuunganisha."

Alisema kaulimbiu ya maadhimisho hayo itajulikana kama miaka 10 ya kupigania maslahi ya wote na Zanzibar yenye mamlaka kamili ambayo inaakisi ahadi yao kwa Watanzania ya taifa la wote, maslahi ya wote.

"Na ahadi yetu kwa Wazanzibari ni Zanzibar Mpya, Zanzibar Moja, Mamlaka Kamili," alisema Shangwe.

Kadhalika, alisema kilele cha maadhimisho ya kuanzishwa kwa chama hicho itakuwa Mei 5, mwaka huu na kwamba kabla ya hapo watafanya shughuli mbalimbali ikiwamo za kijamii na kutoa misaada ya kibinadamu kwa wagonjwa na walioathirika na mafuriko.

Alisema mambo mengine ambayo wanatarajia kufanya katika kuadhimisha miaka 10 ni kongamano la vijana ambalo linatarajiwa kufanyika Zanzibar April 21, mwaka huu likilenga kujadili dhima na wajibu wa kundi hilo katika kupigania Zanzibar yenye mamlaka kamili.

Pia wanatarajia kufanya mkutano wa kidemokrasia Moshi mkoani Kilimanjaro Aprili 27 mwaka huu na kuzindua nembo na bendera mpya.

"Pamoja na ushiriki huu wa mikutano na makongamano, wanachana watashiriki shughuli mbalimbali za kijamii kama vile kuchangia damu, kufanya usafi kwenye hospitali na kuwafariji wagonjwa,"alisema Shangwe.

"Mkesha wa ACT-Wazalendo utakuwa Mei 4, mwaka huu Makao Makuu Dar es Salaam na Ofisi Kuu ya chama Zanzibar, mkesha huu utashuhudia kupandishwa kwa bendera mpya za chama na Mei 5 itakuwa ni kilele na sherehe za maadhimisho haya na zitafanyika mkoani Kigoma na Mwenyekiti wa chama, Othman Masoud Othman, atahutubia taifa."

Chamahicho kimetoa rai kwa wanachama wake wote na viongozi nchi nzima, mikoa yote Tanzania kushiriki maadhimisho hayo ya miaka 10 ya kuzaliwa kwa chama hicho chetu kwa kufanya shughuli za kijamii na kupandisha bendera kwenye ofisi zetu zote.

"Tunatoa shime kwa wanachama, wapenzi na mashabiki wa chama kushiriki nasi kusherehekea miaka 10 ya mafanikio makubwa katika ujenzi wa demokrasia ya vyama vingi hapa Tanzania."

## Abaini kasoro huduma afya ya akili

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), imebaini maeneo yenye kuhitaji maboresho zaidi katika utoaji wa huduma bora za afya ya akili nchini na udhibiti wa vifaatiba katika vituo vya afya vya umma.

Ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa utambuzi wa watu wenye matatizo ya akili katika ngazi ya jamii na badala yake ulilenga watumiaji wa dawa za kulevya, wazee, watu wenye ulemavu, watoto walio katika mazingira magumu na waliopata mimba za utotoni.

Aidha, alisema kuna ukosefu wa huduma za kisaikolojia katika ngazi ya jamii na kubaini kutokuwapo kwa huduma za kisaikolojia ngazi ya jamii, huduma za matunzo ya kisaikolojia na usaidizi kutokuingizwa kikamilifu katika mipango, bajeti, sera, programu, afua, na mikakati kwa ngazi zote za vituo vya kutolea huduma za afya.

Amebaini rasilimali zisizotosheleza (wataalamu, miundombinu, vifaatiba, na dawa) na kutopatikana kwa huduma za utengamo katika vituo vya kutolea huduma hizo ambako kulichangiwa na Wizara ya Afya kutokuwa na mpango wa kuajiri wataalam wa afya ya akili na kutokuwapo muundo wa utumishi unaowajumuisha wahitimu wa taaluma ya huduma za afya ya akili.

Pia, alibaini kulikuwa na ukosefu wa huduma za utengamo kwa ajili ya kuendeleza ujuzi, ushirikiano wa jamii, na misaada inayozingatia urejeshaji, na kwamba kati ya mikoa 28, ni mitano ndiyo ilikuwa na vituo vya utengamo kwa ajili ya huduma za afya ya akili.



Naibu Spika na Mbunge wa Ilala, Mussa Azzan 'Zungu' (wa pili kushoto), akimsikiliza Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ohio, Hilal Ally (katikati), aliyekuwa akilalamikia kufungwa kwa njia ya kuingia kwenye makazi yao na maegesho ya magari, wakati wa ziara ya kusikiliza kero za wananchi wa jimbo hilo, jijini Dar es Salaam juzi. Wa (pili kulia) ni Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## CAG abaini 'madudu' ofisi za balozi Tanzania

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2022/23, imebaini 'madudu' katika ofisi za Balozi za Tanzania kwenye nchi mbalimbali ikiwamo gharama kubwa za kodi ya pango ya Sh. bilioni 18.46 kwa majengo ya ofisi na makazi kwenye balozi 39 za Tanzania nje ya nchi.

Katika ripoti hiyo inaonesha ukarabati wa jengo la ofisi ya Balozi Kampala, Uganda haujaanza licha ya kuwa na bakaa ya fedha Sh. bilioni 1.78 tangu mwaka 2018.

Pia, inaonesha gharama za ukarabati wa jengo la zamani la ubalozi wa Tanzania, lililoko Washington ulikuwa na dosari ambapo gharama ya mkataba iliyonukuliwa ilizidi gharama iliyokadiriwa na mshauri elekezi kwa asilimia 94, ukarabati haukujumuishwa katika mpango wa ununuzi wa mwaka.

Aidha, alisema kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani cha asilimia 20 kilichotajwa katika mchanganuo wa gharama za kazi na ambacho kililipwa katika malipo ya awali hakikuwa na uhalisia kwa kuzingatia kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani ya Washington ambayo ni asilimia sita.

CAG alibaini kulikuwa na hatari ya kulipa riba kwa mkandarasi kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya hati za madai (IPCs) Na. 1 na 2 ambazo zilitolewa tarehe 15 Machi 2023 na 05 Mei 2023, mtawalia, na hazijalipwa mpaka sasa. Mkandarasi alikuwa anawasiliana moja kwa moja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pasipo kumtumia Meneja Mradi.

### MADUDU UNUNUZI

Alisema taasisi 25 zilibainika hazikutekeleza mipango yake ya ununuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 565.49, mamlaka nne za maji zilifanya ununuzi wa jumla ya Sh. milioni 537.93 bila kuwa na mipango ya ununuzi ya mwaka; na taasisi sita zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 1.82 bila kujumuishwa katika mipango yao ya ununuzi ya mwaka.

CAG alibaini miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 635.12 ilianza bila kuwa na cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira na kijamii, wakati ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 7.12 kwa taasisi 15 ulifanyika bila kuidhinishwa na bodi za zabuni.

Pia alibaini upungufu kwenye michakato ya utoaji wa zabuni, ambapo taasisi 16 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 149.56 bila kutumia mfumo wa kielekitroniki.

Kadhalika, alisema taasisi sita zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 77.67 bila kutumia njia za ushindani wa bei. Ununuzi wa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 2.16 ulifanyika bila kutumia mikataba na mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.78 haikupekuliwa na Wanasheria.

Alibaini upungufu katika kutimiza majukumu ya kimkataba ambapo taasisi 11 zilichelewa kulipa madai ya Sh. bilioni 38.73 na kutolipa madai ya Sh. bilioni 19.37 ndani ya muda uliokubaliwa.

Wizara ya ujenzi haijalipa riba ya Sh. bilioni 17.48 iliyotokana na uamuzi wa usuluhishi uliofikiwa tangu mwaka 2014, pamoja na riba ya Sh. bilioni 34.82 iliyotozwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kuchelewa kulipa wakandarasi.

Pia, mikataba 46 ya ujenzi ilikosa dhamana za utendaji kazi zenye thamani ya Sh. bilioni 383.76.

Hata hivyo, alibaini Tume ya Madini na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) hazikudai dhamana ya utendaji kazi na malipo ya awali yenye thamani ya jumla Sh. milioni 675.90 kwenye mikataba iliyositishwa.

# AZAM YAIWEKA PABAYA SIMBA MICHUANO YA CAF

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 2-0 ilioupata juzi usiku dhidi ya Namungo FC, kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, umeifanya Azam FC kung'ang'ania nafasi ya pili, ikifikisha pointi 50 na kuiweka njia panda Simba kwenye ushiriki wa Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Azam imenufaika na sare ya bao 1-1 ambayo Simba ilipata Jumamosi iliyopita dhidi ya Ihefu, ambapo sasa imekaa kwenye nafasi ya pili kwa tofauti ya pointi nne, ingawa ipo mbele michezo miwili zaidi ya Wekundu wa Msimbazi hao wanaosuasua, ambao wana mechi ngumu dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga, Jumamosi wiki hii.

**Mabao yote ya Azam yalifungwa na Kipre Junior dakika ya 62 na 84, na kuifanya timu yake si tu kwamba imeongeza pointi tatu, lakini pia imelipa kisasi cha kufungwa mabao 3-1 katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa, Oktoba 27, mwaka jana.**

Kocha wa Azam FC, Youssoph Dabo, amefurahishwa na ushindi huo, akisema kama wakiendelea hivi, basi msimu huu wanaweza kutwaa ubingwa, au kushika nafasi ya pili na kukata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

"Tumeshinda dhidi ya mpinzani mgumu, tulijitahidi kuwadhibiti tangu kipindi cha kwanza, taratibu tukaanza kuushika mchezo, mwanzo wapinzani walikuwa na nguvu kubwa kwa sababu walikuwa wanacheza nyumbani kwao, na kwa sababu walitufunga mzunguko wa kwanza, walitaka kutufunga tena, niliwaambia wachezaji wangu kuwa huu ndiyo wakati, msimu huu tuna nafasi kubwa ya kupata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa kwa msimu ujao, nina furaha sana mimi nawapongeza wachezaji wangu kwa ushindi huu wa ugenini," alisema kocha huyo.

Iwapo Azam itafanya vema katika mechi zake zinazobaki na Simba ambayo ipo kwenye nafasi ya tatu itaendelea kusuasua, basi inaweza kukata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao, na kuiacha Simba ikienda kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Wakati Azam ikiwa imecheza mechi 22 na kujikusanyia pointi 50, Simba imecheza mechi 20, na kuvuna pointi 46, ambapo kwa mwenendo wa ligi unavyokwenda timu hizi mbili zinaonekana kuwania zaidi nafasi ya pili ambayo inatoa tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Balozi wa Parimatch, Haji Manara (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Erick Gerald (kulia) na Meneja wa Masoko, Levis Paul katika hafla ya kumtambulisha iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




# *Manara sasa balozi mpya Parimatch*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri ya Parimatch Tanzania imemtambulisha rasmi Haji Sunday Manara 'El Bugati' kuwa balozi wao mpya.

Ujio wa Manara umeelezewa kuwa mzuri kwa kampuni hiyo yenye ofa za kijanja na tovuti ambayo inamuonekano mzuri na kasi kubwa ya intaneti.

Akizungumza katika hafla hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu Masoko wa Parimatch, Levis Paul, alisema Manara atawasaidia sana kuitangaza na wateja wao kuweza kushea mikeka yao kwa marafiki ili nao waweze kupata burudani ya kampuni hiyo.

"Tumechukua hatua ya uthubutu na kumchagua Haji Sunday Manara kama balozi wetu kwa ajili ya kuzidi kupata burudani. Yeye ni mtu ambaye amepambana na ameweza kwa upande wake kulizungumzia vema soka la Tanzania bila ya kusahau kuwapa thamani wachezaji wetu wa ndani na wa kimataifa pindi wanapocheza katika ardhi yetu", alisema Paul.

"Kupitia balozi wetu tuna hakika ataipeperusha vema Chapa ya Parimatch kila eneo pamoja na kusaidia kutoa uelewa kwa wachezaji maana halisi ya kubeti ili wote tuweze kufurahi na kucheza kistaarabu."

Kwa upande wa Manara, alisema: "Kiukweli nilipigiwa simu na kampuni nyingi, lakini katika uchunguzi wangu nikabaini kuwa Parimatch ndio kampuni bora kwangu kufanya nayo kazi kwa sababu inaaminika duniani kote na katika hili nyinyi mtakuwa mashahidi wa hili.

"Msimu uliopita walikuwa wameidhamini Klabu ya Mbeya City iliyokuwa inashiriki ligi yetu pendwa ya Tanzania na kwa msimu huu klabu mbili zinadhaminiwa na kampuni hii.

"Ukiachilia mbali masuala ya soka, hawa Parimatch pia wanathamini sana vipaji vya muziki na vichekesho vya vijana wetu na ndio sababu mnawaona hapa hawa vijana wenzangu tupo pamoja hapa. Mbali na hilo hii ndio kampuni kinara kwa michezo ya kubashiri mtandaoni na inapatikana katika zaidi ya nchi 15 duniani na ikiwa na wateja zaidi ya milioni.

"Napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha nanyi ndugu zangu wapenda michezo ya soka kuja kujiunga na familia kubwa ya Parimatch kwani ukiwa huku utafurahi kwa malipo ya papo hapo, 'Odds' kubwa na masoko ya kila aina, yaani ushindwe wewe tu."

"Kwa kumalizia niwakumbushe Watanzania pamoja na wadau wote wa kubeti kuwa Kampuni ya Parimatch ndio kinara wa michezo ya kubashiri mtandaoni na imekuwa ikitoa ofa kubwa ya bonasi ya Ukaribisho ya 125% hadi kufikia TZs 1,000,000 kwa wateja wapya wanaojiunga nao!" aliongeza kusema.

## Kuogelea Taifa rasmi J'mosi

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Taifa ya Klabu ya mchezo wa Kuogelea yanatarajiwa kuanza Aprili 20-21, mwaka huu, katika bwawa la kuogelea la Shule ya Kimataifa Tanganyika iliyopo Masaki, Dar es Salaam, imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Ufundi wa Chama cha mchezo wa Kuogelea Tanzania (TSA), Amina Mfaume, alisema lengo la mashindano hayo ni kupata waogeleaji watakaounda Timu ya Taifa itakayokwenda kushiriki mashindano ya Kanda ya Tatu yatakayofanyika baadaye mwaka huu nchini Burundi.

Alisema mpaka sasa tayari Klabu 11 zimethibitisha kushiriki ambapo 10 ni kutoka mikoa ya Tanzania na moja kutoka jijini Nairobi, Kenya.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kuelekea kwenye mashindano hayo tunaomba taasisi na kampuni mbalimbali zijitokeze kutuunga mkono ili tuweze kufanikisha mipango yetu," alisema Mfaume.

## Singida FG yalia na mabeki kipigo Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Singida Fountain Gate, limelia na safu yake ya ushambuliaji baada ya kupokea kichapo cha mabao 3-0 dhidi ya Yanga juzi.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ngawina Ngawina, aliliambia Nipashe jana kuwa wamepoteza mchezo huo kutokana na makosa yaliyofanywa na mchezaji mmoja mmoja, pamoja na uwanja kujaa maji.

Alisema licha ya matokeo hayo wachezaji wake walionyesha uwezo mzuri katika mchezo wao huo na kuweka wazi kuanza kuyafanyia kazi makosa yaliyojitokeza ili kupata matokeo mazuri kwenye michezo ijayo.

"Hatukutegemea kupata matokeo hayo, tumefungwa kwa uwezo wa mchezaji mmoja mmoja vile vile uwanja ulikuwa umejaa maji yaliyosababisha wachezaji wetu washindwe kucheza vema mpira," alisema Ngawina.

Alisema kwa sasa anaelekeza nguvu zake kwenye mchezo wao ujao dhidi ya Mashujaa FC utakaopigwa Aprili 21, mwaka huu jijini Mwanza.

## ZISIKUPITE

### ZIDANE ATAJWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imewasiliana na Zinedine Zidane, ambaye bado hajarejea kwenye uongozi wa timu tangu aondoke Real Madrid miaka mitatu iliyopita, ili kupima nia yake ya kurithi mikoba ya Thomas Tuchel mwishoni mwa msimu huu. ***(Marca)***

### KOVAC AIBUKIA LIVERPOOL

KOCHA wa zamani wa Bayern Munich, Monaco na Wolfsburg, Niko Kovac, ameibuka kama kocha anayetarajiwa kumrithi Jurgen Klopp katika Klabu ya Liverpool. ***(Mail)***

### GIBBS-WHITE ALENGWA

KLABU ya Newcastle United imemfanya kiungo mshambuliaji wa Nottingham Forest, Morgan Gibbs-White mwenye umri wa miaka 24, kuwa mmoja wa wachezaji inaowalenga msimu ujao. ***(Mirror)***

### EDWARDS AWANIWA LIVER

LIVERPOOL inaweza kumsajili winga, Marcus Edwards mwenye umri wa miaka 25, kutoka Sporting Lisbon kwa pauni milioni 30 msimu huu. ***(Football Insider)***

### RASHFORD KUBAKI UNITED

MCHEZAJI Marcus Rashford anatazamiwa kubakia Manchester United huku Paris St-Germain ikiweka wazi kuwa haina nia ya kumsajili mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 26. ***(Sun)***

### KOOPMEINERS ATAJWA

CHELSEA inatayarisha ofa ya kumnunua kiungo wa kati wa Uholanzi, Teun Koopmeiners mwenye umri wa miaka 26, baada ya kutuma maskauti kumwangalia wakati wa ushindi wa Atalanta wa Ligi ya Europa dhidi ya Liverpool. ***(Sportmediaset - Via italia)***

### DEWSBURY-HALL AFUATILIWA

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia kiungo wa kati wa Leicester City, Kiernan Dewsbury-Hall na wanaweza kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kwa kati ya pauni milioni 30 na pauni milioni 40 msimu huu. ***(Football Insider)***

### CALAFIORI AMULIKWA SPRURS

KLABU ya Tottenham pia ina nia ya kumsajili beki wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 21, kutoka Bologna msimu wa majira ya joto. ***(Tuttosport)***

### GIL KURUHUSIWA KUONDOKA

WINGA wa Hispania, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 23, anaweza kutaka kuondoka Tottenham Hotspur msimu ujao na tayari anaweza kuruhusiwa kuchapa mwendo kwa uhamisho wa kudumu. ***(Give Me Sport)***

### DENDONCKER LULU EVERTON

EVERTON inataka kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji, Leander Dendoncker mwenye umri wa miaka 28, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Napoli, kutoka Aston Villa msimu huu. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: VIJANA SIMAMENI NAFASI ARSENAL BADO IPO

**LONDON,** England

**Hatuna suluhu nyingine, ukitaka ubingwa lazima ushindi, sasa ni mtihani mkubwa...**

MIKEL Arteta amewataka wachezaji wake wa Arsenal kusimama na kuhakikisha matokeo ya mchezo mmoja yasiharibu msimu wao baada ya kupokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Aston Villa Jumapili kwenye Uwanja wa Emirates.

**Mabao ya Leon Bailey na Ollie Watkins yaliwafanya 'Washikabunduki' hao kupoteza kwa mara ya kwanza kwenye Ligi England tangu mkesha wa Mwaka Mpya na inamaanisha Manchester City inaweza kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu kwa mara ya tano katika misimu sita ikiwa itashinda mechi zake sita za mwisho.**

Arsenal sasa wanakabiliwa na mchezo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich Jumatano, ambapo mechi yao ya kwanza walitoka sare ya mabao 2-2, kabla ya safari dhidi ya Wolverhampton Wanderers, ambao waliwafunga Man City na Tottenham Hotspur nyumbani mapema msimu huu.

Alipoulizwa kama msimu wao tayari umeyumba, Arteta alijibu: "Ikiwa matokeo ya mchezo mmoja yatafanya hivyo, basi hatuna nguvu za kutosha. Hiyo ni rahisi sana. Tulikuwa na moja ya matokeo bora ambayo tumekuwa nayo msimu wote dhidi ya timu nzuri sana.

"Ilipaswa tuwe mbele kwa mabao matatu, manne au zaidi, haikutokea, na kipindi cha pili kasi ilibadilika, hatukuweza kudhibiti na kuzalisha kile tulichofanya kipindi cha kwanza. Tuliruhusu mabao mawili mabaya sana na tukapoteza mchezo.

"Unaposhinda na kushinda na kushinda kwa miezi minne ni rahisi sana kufanya hivyo. Wakati wa kufanya hivyo ni sasa.

"Hatuna suluhu nyingine. Ukitaka kutwaa ubingwa, ukitaka kuwapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ukiwa na wakati huu lazima usimame. Ikiwa sivyo, hiyo ina maana kwamba huna ubora ambao ni muhimu sana. Sasa ni mtihani mkubwa kwetu."

HABARI MICHEZO




# MCHEZAJI AANGUKA, MCHEZO WAAHIRISHWA

**ROME,** Italia

MLINZI wa AS Roma, Evan Ndicka, alianguka uwanjani katika kipindi cha pili cha mechi yao ya Ligi Kuu Italia, Serie A, dhidi ya Udinese Jumapili na kulazimika kutolewa nje kwa machela, huku mechi ikiahirishwa.

Matokeo yalikuwa 1-1 pale mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ivory Coast alipoanguka uwanjani dakika 18 kabla ya mchezo kumalizika.

Ndicka alikuwa na fahamu, lakini alionekana wazi kuwa na maumivu, akipapasa kifua chake kwa mkono wake wa kulia huku timu ya madaktari ikimkimbilia.

Kisha alibebwa, akitoa ishara ya dole gumba.

"Kufuatia dharura ya matibabu ya uwanjani iliyomhusisha Evan Ndicka, mechi kati ya Udinese na Roma imesimamishwa," ilisema taarifa ya Roma kupitia mtandao wa Kijamii wa X.

"Mchezaji huyo ana fahamu na amepelekwa hospitali kwa uchunguzi zaidi."

Baada ya kuchelewa kwa muda mrefu, mechi ilisimamishwa, na wachezaji wakaondoka uwanjani.

Vyombo vya habari vya Italia viliripoti kuwa vipimo vilivyofanywa kwa Ndicka katika hospitali hiyo vimesema haukuwa mshtuko wa moyo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alibaki hospitalini kwa uchunguzi.

"Kikosi kilienda kumtembelea Ndicka hospitalini. Evan anajihisi vizuri na yuko katika hali nzuri," klabu hiyo ilisema kwenye X.

"Atabakia hospitalini kwa uchunguzi zaidi"

# Klopp haelewi kwa nini Liver inayumba

**LIVERPOOL,** England

MSIMU wa Liverpool umeanza kuyumba, na kocha Jurgen Klopp amesema anashindwa kueleza ni kwa nini.

Kipigo cha bao 1-0 cha nyumbani kutoka kwa Crystal Palace kiliharibu nafasi ya kutoa changamoto ya kuwania taji la Ligi Kuu England Jumapili, siku tatu baada ya kucharazwa mabao 3-0 na Atalanta katika Uwanja wa Anfield kwenye mchezo wa mkondo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Europa.

Kupoteza huko mfululizo nyumbani kumekuja baada ya sare ya Jumapili iliyopita na Manchester United katika Uwanja wa Old Trafford na kuwaacha vijana wa Klopp wakiwatazama viongozi Manchester City wakiwa juu.

"Inawezekana," Klopp alisema, alipoulizwa ikiwa kupoteza kwa Palace kulitokana na kuchoka kwa kipigo kutoka kwa Atalanta.

"Ukiangalia timu yangu kwa miaka mingi, nadhani unaweza kusema kwamba shinikizo letu kwa kawaida ni zuri. Kipindi cha kwanza (dhidi ya Palace), tulikuwa na nafasi nyingi - lakini imewezaje kutokea?

"Ni siku chache tu zilizopita ambapo tulicheza mchezo mbaya, kwa hiyo inaweza kuwa na kitu cha kufanya na hilo. Kwa kweli ulikuwa mchezo mzuri sana. Lakini si rahisi hivyo kwa bahati mbaya."

Eberechi Eze alifunga bao akiunganisha pasi ya Tyrick Mitchell dakika ya 14 na kuifanya Liverpool kupoteza kwa mara ya kwanza kwenye ligi katika uwanja wa Anfield katika mechi 28 -- kuanzia Oktoba 2022.

# Alonso, Leverkusen wabeba kombe baada ya miaka 120



**LEVERKUSEN,** Ujerumani

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, alisifu ushindi wao kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kama "kitu cha ajabu" baada ya kutwaa kombe lao la kwanza katika historia ya miaka 120 ya klabu hiyo Jumapili jioni.

Leverkusen walikuwa na uongozi wa pointi 13 kuelekea mechi dhidi ya Werder Bremen, wakijua ushindi ungeihakikishia kutwaa ubingwa wa Bundesliga huku zikiwa zimesalia mechi tano.

Wenyeji walifanya kazi rahisi kwa Bremen waliposhinda mabao 5-0 shukrani kwa mkwaju wa penalti kutoka kwa Victor Boniface, mkwaju mzuri wa Granit Xhaka na hat-trick ya Florian Wirtz.

Ushindi huo uliashiria mwisho wa mbio za Bayern Munich za kutwaa taji hilo mara 11 mfululizo, na mafanikio kwa Leverkusen baada ya kukaribia sana kulitwaa taji hilo mwaka 2000 na 2002.

"Huu ni wakati maalum kwa klabu," alisema Alonso baada ya mechi.

"Baada ya miaka 120, tunashinda Bundesliga kwa mara ya kwanza ni jambo la ajabu. Wachezaji walifanya vizuri, walikuwa timu ya juu pamoja. Ninajivunia wote. Kwangu ni heshima kufanya kazi hapa.

"Mwisho tunaweza kusema Bayer Leverkusen ni bingwa wa Ujerumani. Ni heshima kubwa kwetu sote. Umepatikana kwa sababu ya timu na mashabiki. Kila mtu, idara zote, walikuwa wakifanya kazi na kupigania taji hili.

"Kwa hiyo sisi ni matokeo ya kazi hiyo ngumu kwa miaka mingi. Huu ni wakati wa kufurahia mafanikio makubwa kwa klabu hii kila wakati ni maalum kwa kila mtu.

Alipoulizwa ni lini alifikiri taji hilo lingeweza kufikiwa, alibainisha ushindi wao dhidi ya Bayern Munich mnamo Februari 10, ambao uliipa Bayer uongozi wa pointi tano kileleni mwa Bundesliga.

Hadi siku ya mechi ya 29 inakaribia, Bayer Leverkusen walikuwa pointi 16 mbele ya Bayern.

Leverkusen walipofunga katika historia, mashabiki walivamia uwanja mara mbili katika dakika 10 za mwisho.

Uvamizi wa kwanza mdogo ulikuja baada ya Wirtz kufunga la pili, na la nne la Leverkusen, dakika ya 83.

Wirtz walipofunga bao la tatu na la tano dakika ya 89, uvamizi ulikuwa mkubwa zaidi. Mwamuzi alisubiri dakika ya 90 huku mashabiki wakiwa bado uwanjani, akapuliza filimbi kumaliza mchezo.

"Mashabiki walikuwa juu," Alonso alisema. "Walijipanga njia nzima hadi uwanjani. Tuliweza kuona kwamba walitaka hili na tulilizungumza kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, kwamba tulitaka kubadilisha nguvu zao uwanjani."

HABARI MICHEZO

# NBC, YANGA WAZINDUA KADI ZA KIMATAIFA ZA UANACHAMA

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), kwa kushirikiana na Klabu ya Soka ya Yanga wamezindua kadi za kimataifa za uanachama wa klabu hiyo inayofahamika kama 'NBC Yanga Membership Card'.

**Hatua hiyo inatajwa kuwa pamoja na faida nyingine inalenga kurahisisha malipo ya uanachama kwa wanachama wa klabu hiyo, hivyo kusaidia kuongeza mapato ya klabu.**

Uzinduzi wa kadi hizo ulifanyika jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla fupi iliyohusisha viongozi waandamizi wa pande zote mbili, wafanyakazi benki hiyo, wanachama na mashabiki mashuhuri wa Klabu ya Yanga. Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Steven Mnguto, akimwakilisha rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia.

Katika kusaini makubaliano ya utekelezaji wa mpango huo, ilishuhudiwa Rais wa Klabu ya Yanga, Mhandisi Hersi Saidi, akiongoza zoezi hilo kwa niaba ya klabu hiyo huku upande wa Benki ya NBC, ukiongozwa na Mkurugenzi wa Biashara wa benki hiyo, Elvis Ndunguru, aliemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Ndunguru alisema kama mdhamini mkuu wa Ligi ya soka Tanzania (NBC Premier League), Ligi Daraja la Kwanza (NBC Championship) na Ligi ya Vijana (NBC Youth League), benki hiyo imedhamiria kuonyesha kwa vitendo nia yake ya kuleta mapinduzi halisi kwenye mchezo wa soka nchini kwa kuwekeza zaidi katika huduma mbalimbali zinazolenga kuboresha uendeshwaji wa klabu zinazoshiriki ligi hiyo ikiwamo suala zima la usajili wa wanachama.

"Kadi hii tunayoizindua leo, imeambatana na faida nyingi ambazo wanachama wa Yanga watanufaika nazo ikiwamo urahisi wa kununua tiketi za mechi za timu yao za NBC Premier League, FA na CAF Champions League kwa mfumo wa N-Card. Wanayanga sasa hawatahitaji tena kununua N-Card kwa kuwa kadi hizi tayari zimeunganishwa na mfumo wa N-Card. Kadi hii pia inaweza kutumika kufanya malipo katika vituo vyote vya TAMESA nchini ikiwamo malipo ya huduma ya Ferry -Kigamboni."

"Zaidi pia kupitia kadi hii wanachama wa Yanga watapata urahisi wa kutoa fedha kupitia mashine za fedha (ATMs) popote duniani, kufanya malipo bure kupitia mashine za malipo (POS) popote duniani, urahisi wa kufanya malipo ya mtandaoni yaani (online paymeunt) na urahisi wa kufanya malipo ya kidijitali kupitia mifumo ya NBC Kiganjani na Internet Banking," alifafanua.

Kwa mujibu wa Ndunguru, kadi hizo ambazo zina viwango vya kimataifa vya ulinzi na usalama, zitapatikana maeneo mbalimbali ikiwamo matawi yote 67 ya Benki ya NBC na mawakala wa benki hiyo zaidi ya 60,000 waliopo nchi nzima.

"Mbali na kuwapa wanachama wa Yanga uwezo wa kufikia fedha zao saa 24 ndani na nje ya nchi kwa kupitia mtandao mpana wa Benki ya NBC, kadi hii pia ina faida kadhaa ikiwamo uwezo wa kufanya malipo mbalimbali iksms Netflix, DSTV, AZAMTV na mengineyo, punguzo la bei ndani na nje ya nchi kupitia wadau wa biashara wa Benki ya NBC, malipo ya kidigitali yaani (tap and pay) ambayo ni huduma mpya nchini, usalama uliobreshwa kupitia teknolojia ya 3D na kubwa kuliko yote kadi hii pia itatumika kama kadi ya uanachama wa Klabu ya Yanga (Wananchi)." aliongeza.

Awali akizungumza kwenye hafla hiyo, rais wa Yanga, Hersi alisema klabu hiyo inajivunia kuingia makubaliano hayo na Benki bora ya NBC Tanzania na kwamba hatua hiyo itaisadia sana katika kuwahudumia wanachama wake hususan kwenye usajili na kutoa kadi za Uanachama.

"Ukijiunga kuwa Mwanachama wa Yanga, kupitia Benki ya NBC utapata kadi ya Uanachama na hapo hapo utapata huduma za kibenki. Lakini kubwa zaidi kadi ya NBC imeunganishwa na huduma za N-CARD hivyo Mwanachama wetu atapata huduma ya kuingia Uwanjani pamoja na huduma za usafiri," alibainisha.




Rais wa Klabu ya Yanga, Mhandisi Hersi Saidi (aliyeshika bango kulia), Mkurugenzi wa Biashara wa benki ya NBC , Elvis Ndunguru (aliyeshika bango kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Steven Mnguto (katikati yao) wakifurahia pamoja na wanachama wa klabu hiyo wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa kadi za kimataifa za uanachama za Klabu ya Yanga zinazofahamika kama 'NBC Yanga Membership Card'. Uzinduzi huo ulifanyika jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Serikali kuunga mkono juhudi soka la vijana

**Na Saada Akida**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, amesema kuwa serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), haitakubali kuona juhudi zinazoletwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Ulimwenguni (FIFA), katika maendeleo ya soka la vijana nchini kuanzia ngazi ya chini zikitoweka.

Kauli hiyo aliitoa jana katika uzinduzi wa program ya mpira wa miguu kwa ajili ya watoto kwenye shuleni iliyoandaliwa na TFF kwa kushirikiana na FIFA na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa ajili ya mafunzo kwa walimu 46 wa shuleni za msingi kutoka wilaya 16 nchini. Msigwa alisema walimu waliopata mafunzo hayo wanatakiwa kuzingatia kwa sababu hiyo ni fursa ambayo imepata nchini kwa kutoa elimu shuleni ili ujuzi huo waupate watoto.

Alisema program hiyo imekuja kimkakati kwa sababu nchini imewekeza katika michezo na kuanzia chini hana budi kuipongeza TFF kuwa karibu na uhusiano mzuri na Fifa na CAF.

"Kwa sasa hatutalala na kukubali kuona juhudu hizi zinapotea, kwa sababu TFF wanafanya kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wa FIFA na CAF, walimu waliopata program hizi wahakikishe wanawatengeneza vijana vizuri.Program hii ya mpira shuleni ni kitu muhimu sana kwa sabahu kuna vipaji vingi, lakini hawapati nafasi ila hii inaweza kusaidi kwa taifa letu kwa siku za mbele," alisema Msigwa.

Aliongeza kuwa nchini itakuwa wenyeji wa AFCON 2027, hivyo kunatakiwa kuwa na maandalizi makubwa ikiwamo kuandaa timu za taifa na inaanzia shuleni, kitu ambacho walimu wanatakiwa kutumia vizuri mifumo hiyo maalum kuwapika vijana wa kesho.

Naye Meneja wa program hiyo wa Fifa, Antonio Sanchez, alisema program hiyo ni maalum kwa vijana hao na inafaida mbali na soka mtoto pia atapata elimu ya kujifunza vitu vingine zaidi.

## *Mo afanya kikao kizito mechi Yanga*

INATOKA UKURASA 24

mtoa habari wetu.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema kazi kubwa waliyonayo sasa ni kusaka pointi tatu kwenye mechi dhidi ya Yanga.

"Tunatambua kwamba tuna mechi ngumu, hivyo tupo tayari kwa ajili ya mechi hii tunachoomba ni kwamba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono," alisema.

Simba imecheza mechi nne mfululizo bila kupata ushindi ambapo ilichezwa mbili ya nyumbani na ugenini dhidi ya Al Ahly ya Misri, ikiwa ni robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikifungwa bao 1-0 nyumbani, na mabao 2-0 ugenini, na ikatolewa kwenye michuano ya FA kwa mikwaju ya penalti 6-5 dhidi ya Mashujaa FC baada ya sare ya bao 1-1 dakika 90 za mchezo, kabla ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Ihefu, mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Jumamosi iliyopita.

Inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 46 kwa michezo 20 ambayo imecheza mpaka sasa.

## Yanga SC yaonya mashabiki

INATOKA UKURASA 24

uwanjani.

Kwa munibu wa rais wa Yanga, Mhandisi Hersi Said, alisema Yanga inajivunia kuingia makubaliano na Benki bora ya NBC kwenda kuwahudumia wanachama wao kwenye usajili na kutoa kadi za uanachama.

Alisema ukijiunga kuwa mwanachama wa Yanga, hapo hapo utapata huduma za kibenki, lakini kubwa zaidi kadi ya NBC imeungajishwa na huduma za N-CARD, hivyo mwanachama wa Yanga atapata huduma ya kuingia uwanjani pamoja na huduma za usafiri

# Michezo

Jumanne Aprili 16, 2024

**Nipashe**



**'Ubingwa Arsenal bado upo'** UKURASA 21

**KIKAO CHA DHARURA...**



Mwekezaji na Rais wa Heshima wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wakiwa kwenye kikao kujadili mwenendo timu hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# Mo afanya kikao kizito mechi Yanga

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

●●● Wachezaji Simba nao wawekwa kitimoto, lengo ni kuhakikisha...

MWEKEZAJI na Rais wa Heshima wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, amefanya kikao kizito na Bodi ya Wakurugenzi kutokana na mwenendo mbovu wa timu hiyo, huku Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, akiwaweka kitimoto wachezaji wake kujua tatizo lipo wapi ili kuweka mambo sawa kuelekea katika mechi ya Jumamosi wiki hii dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga.

**Taarifa za uhakika zilizoifikia Nipashe jana, kutoka ndani ya Bodi ya Wakurugenzi Simba, imeeleza kuwa baada ya kuondolewa kwenye Kombe la FA, na kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Ihefu FC, viongozi, benchi la ufundi la wachezaji walikuwa na kikao cha pamoja wakiongozwa na Mo mwenyewe, ambacho lengo lake ni kujua tatizo ni nini na linaanzia wapi na namna ya kulirekebisha.**

Mtoa habari anasema kulikuwa na ajenda mbili, kwanza ni kwa nini timu inashindwa kupata matokeo katika mechi zake kadhaa za hivi karibuni, lakini pia mipango ya kuelekea mchezo wa Jumamosi dhidi ya Yanga.

Mo, mwenyewe ameposti picha kwenye akaunti yake ya instagram, ambayo inaonyesha yupo kwenye kikao na baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo na kukiri kufanya hivyo, akiwataka wanachama na mashabiki wa Simba wasife moyo.

"Nimefanya kikao na viongozi wa Simba kujua changamoto zipo wapi na namna ya kuzitatua. Kikao kimeenda vizuri, Wanasimba tusife moyo, tuendele kushirikiana," aliandika rais huyo.

Habari zinasema kuwa mara baada ya kikao hicho, Benchikha naye akawa na kikao chake na wachezaji bila kuwahusisha viongozi.

"Ni kweli baada ya kikao cha bodi kikiongozwa na Mo mwenyewe, kocha alifanya kikao kingine na wachezaji wake tu bila ya kuwapo kwa kiongozi yeyote na kuzungumza nao na kuweka mipango yao kuelekea mechi dhidi ya Yanga.

Kocha hataki kupoteza mechi dhidi ya Yanga mara mbili, na amewataka wachezaji kuwa makini ikiwamo safu ya ushambuliaji na ulinzi kutowapa nafasi ya wapinzani kufika katika eneo, lakini pia amerejesha morali ya wachezaji," kilisema chanzo hicho.

Ikumbukwe katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Novemba 5, mwaka jana, Simba ilipata kipigo cha fedheha cha mabao 5-1, Uwanja wa Benjamin Mkapa, hivyo kumekuwa na hofu kubwa ya kupata kichapo kingine kikubwa kutokana na mwenendo usioridhisha wa timu hiyo, huku wanachama na mashabiki wake wakiwa wamekata tamaa.

Pia kilisema kuna uwezekano mkubwa timu kwenda kuweka kambi nje ya Dar es Salaam kwa ajili ya mechi hiyo.

"Timu inaweza kutoka Dar es Salaam, itakwenda kuweka kambi nje kama mipango itakaa sawa, kokote kule hata Zanzibar kama tulivyofanya wakati wa kujiandaa na Al Ahly," alisema

# Yanga yaonya mashabiki 'dabi' Simba Jumamosi

**Na Saada Akida**

MSEMAJI wa Yanga, Ali Kamwe, amesema licha ya Simba kupitia kipindi kigumu cha kutopata matokeo mazuri, lakini wanaitazama timu hiyo katika mambo matatu muhimu kuelekea mchezo wa Derby utakaopigwa Jumamosi wiki hii.

Kikosi cha Yanga kilirejea jana kutoka jijini Mwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Singida Fountain Gate ambayo kilishinda mabao 3-0, na leo kinaingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo wa Kariakoo 'Derby', ambao utapigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam saa 11:00 jioni.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamwe alisema anewataka mashabiki kuachana na fikra ya kuwa mpinzani wao amechoka na hajapata matokeo mazuri bali wanatakiwa kufikiria namna ya kuzipata pointi tatu mbele ya Simba. Alisema mechi ya Simba na Yanga ina umuhimu wake, na kwamba haitakiwi kwenda uwanjani na mawazo ya pointi tatu kwa kufikiri mpinzania wao amechoka, jambo ambalo wanatakiwa kuliondoa kichwani na kutambua wanaenda kukutana na timu tishio.

"Hatuitazamani Simba kama wanavyotazama mashabiki, bali kwetu ni timu tishio na tuko nao katika vita, kwa sababu wana wachezaji wazoefu kwenye kucheza Derby kubwa na tofauti pia viongozi makini na wenye mipango na ubora wa hizi mechi," alisema Kamwe.

Aliwataka mashabiki wa Yanga, kuwa kujitokeza uwanjani na kuifanya Kariakoo Derby kuwa kama Kilele cha Siku ya Wananchi kwa kujaza uwanja na kutowapa nafasi ya wapinzani wao kuwa wengi.

"Asitokee Mwanayanga akabaki nyumbani na baada ya matokeo akajisifia, tunahitaji siku hizo kuwa ni Kilele cha Siku ya Wananchi na tusiwape nafasi mashabiki wa upande wa pili kuwa wengi," alisema Kamwe.

Kuhusu majeruhi, alisema baadhi ya wachezaji wamerejea akiwamo Kennedy Musonda na Pacome Zouzoua yuko katika hatua nzuri ya kurejea katika hali yake ya kwaida.

"Hatuwezi kuwalazimisha wachezaji kucheza kwa sababu Yang ina kikosi kipana na tunaenda siku hiyo kwa roho ya kikatili," alisema Kamwe.

Katika hatua nyingine Yanga kwa kushirikiana na Benki ya NBC, wamezindua kadi ya wanachama wa klabu hiyo ambayo itawasaidia katika mambo mbalimbali ikiwamo kuingia

INAENDELEA UKURASA 23



Msemaji wa Yanga, Ally Kamwe.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >